SportPesa
TZS. 823,998,440
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**TANESCO** yarudisha gharama za awali kuunganisha umeme
UKURASA 4



**DSTV YATAMBULISHA PANDA TUKUPANDISHE**
UKURASA 20

Nipashe
Alhamisi Januari 6, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579817
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Mauaji yatikisa

UKURASA 2 & 10

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**LATRA YAINGILIA KERO USAFIRI MIKOA KASKAZINI KWENDA DAR**
KUTOKANA na abiria wanaoelekea Dar es Salaam kutoka mikoa ya Kanda ya Kaskazini kuongezeka, Mamlaka ya Udhibiti

UKURASA WA 5
**MIAKA MITANO JELA KUUA SHEMEJI BILA KUKUSUDIA**
MAHAKAMA Kuu Masijala ya Sumbawanga imemtia hatiani na kumhukumu kifungo cha miaka mitano jela David...

UKURASA WA 7
**WATU 32 WAFARIKI MATUKIO YA MOTO**
WATU 32 wamefariki dunia na wengine 145 wamejeruhiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka jana...

## Mwinyi afunda mabalozi sera diplomasia na uchumi wa bluu

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akisisitiza jambo alipozungumza na mabalozi walioteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali walipofika Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**



## Presha, kihoro vyapanda vigogo kusudio Rais kufanya mabadiliko

UKURASA 3

MICHEZO WANAYANGA KUJIANDIKISHA KISASA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Watu watano wafa kwa radi

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

WATU watano wa kijiji cha Kibuye, Kibondo mkoani Kigoma wamefariki dunia baada ya kujeruhiwa na radi kutokana na mvua kubwa iliyonyesha ikiambatana na radi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kigoma, James Manyama, alisema jana kuwa tukio hilo limetokea juzi majira ya saa 12:00 jioni na kusababisha vifo vya watoto wanne wanaokadiriwa kuwa na miaka mitano na 10 na mwanamke mwenye miaka 50.

Aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Baseka Japhet (10) mwanafunzi wa darasa la tano, Goma Jeremia (5), Rock Ramadhani (5), Alam Paschal (9) na Anatoria Muhoza (50), mkulima mkazi wa kijiji cha Kibuye.

Kamanda alisema watoto hao walikuwa nyumbani wanacheza chini ya mti wa mwembe wakati mvua inaendelea kunyesha ndipo walipopigwa na radi na kusababisha vifo vyao, huku Muhoza akipigwa na radi akiwa shambani akiendelea na shughuli za kilimo.

Alisema miili ya marehemu wote imehifadhiwa Hospitali ya Wilaya ya Kibondo kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Manyama alitoa wito kwa wananchi wote wa Mkoa wa Kigoma hasa katika kipindi hiki cha mvua, kujikinga ndani ya nyumba zao na waepuke kujikinga mvua chini ya miti.

# Mauaji yatikisa kila kona

**Na Maulid Mmbaga**

MAUAJI ya watu yameripotiwa katika maeneo mbalimbali kutokana na baadhi ya watu kuwaua wenzao kinyama, huku wengine wakipoteza maisha kutokana na majanga mbalimbali ikiwamo kufa kwa kupigwa radi.

Matukio hayo yametokea ndani ya muda usiozidi wiki moja katika mikoa mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, Rukwa, Katavi na Kigoma.

Jijini Dar es Salaam, mwendesha pikipiki ya abiria, maarufu kama bodaboda, aliyejulikana kwa jina moja la Erick, anadaiwa kuchinjwa kwa kutenganishwa kichwa na kiwiliwili na watu wasiojulikana kisha kuporwa pikipiki na kutoweka kusikojulikana.

Tukio hilo lilitokea jana mtaa wa Kibulului, Goba, wilaya ya Kinondoni usiku wa kuamkia jana, na limethibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Ramadhani Kingai.

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Kamanda huyo alisema kijana huyo ni dereva bodaboda anayeegesha eneo la Goba, alikutwa amechinjwa na watu wasiojulikana.

"Ni kweli tukio limetokea na tayari tumeshaanza kukamata baadhi ya washukiwa, tunaendelea na uchunguzi na utakapokamilika tutatoa taarifa kwa umma,"alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda huyo, wauaji hao baada ya kutekeleza tukio hilo walitelekeza mwili barabarani na kukimbilia kusikojulikana.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kibululu Goba, Sadiki Mtanga, alisema kijana huyo alikuwa ni mkazi wa mtaa wake akijishughulisha na kuendesha pikipiki.

"Watu waliosababisha kifo cha kijana huyo wanadaiwa kuwa ni wale wanaojihusisha na wizi wa bodaboda, japo bado hawajajulikana kuwa ni wakazi wa wapi. Nawasihi madereva kuwa makini nyakati za usiku wasimuamini kila mtu kwani wengine wanakuwa na nia mbaya," alisema Mtanga.

Aliongeza kwa kuwataka wananchi kuwa watulivu wakati wanashirikiana na Polisi kuchunguza ili kuwabaini waliohusika na tukio hilo, huku akiomba ushirikiano wa jamii kuwakamata wahusika.

Mmoja wa wananchi wa eneo hilo, Salimu Bakari alieleza kuwa dereva bodaboda huyo alifanyiwa kitendo cha kinyama akidai kuwa watuhumiwa walimkata mwili wake bila huruma hali ambayo kwa upande wao hawakuridhishwa nayo.

Alidai kuwa kumekuwa na wizi unaoendelea katika maeneo hayo, huku akitoa wito kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuwafuatilia watu wanaojihusisha na uovu. Kwa kuwa wanarudisha nyuma maendeleo.

"Hawa watu kitu wanachokifanya ni kinyume na sheria na hakikubaliki katika jamii yetu, waendesha pikipiki wawe makini na watu wanaowakodisha akiona haielewi sehemu mteja wake anayomuelekeza ampeleke ni bora aache au amuambie atafute usafiri mwingine kwa ajili ya usalama wake,"alishauri Bakari.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimjulia hali Mufti na Shekhe Mkuu wa Tanzania, Abubakar Bin Zubeir ambaye amelazwa katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) mkoani Dar es Salaam kwa matibabu. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Samweli Swai. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mwinyi awafunda mabalozi wapya diplomasia ya uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameeleza haja kwa mabalozi wanaoiwakilisha nchi nje walioteuliwa hivi karibuni, kuipa kipaumbele sera ya diplomasia ya uchumi katika nchi wanazokwenda kufanya kazi.

Dk. Mwinyi alieleza hayo jana, Ikulu Zanzibar, alipokutana na kufanya mazungumzo na mabalozi hao.

Baadhi ya mabalozi hao na nchi wanazokwenda kuiwakilisha Tanzania ni Perera Ame Silima (Visiwa vya Comoro), Said Shaib Mussa (Kuwait), Fredrick Kibuta (Urusi), Prof. Adelardus Kilangi (Brazil), Alex Kalua (Israel) na Said Mshana Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Rais Dk. Mwinyi aliwaeleza mabalozi hao kwamba sera ya diplomasia ya uchumi ndiyo iliyopewa kipaumbele hivi sasa katika Tanzania, hivyo ni vyema wakaenda kuifanyia kazi ili uchumi wa Tanzania uzidi kuimarika.

Rais Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kuwaeleza mabalozi hao namna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilivyoweka mikakati yake katika kuimarisha uchumi wake ambao dira ni uchumi wa buluu.

Alisema utalii ni miongoni mwa sekta zilizopewa kipaumbele kupitia uchumi huo wa buluu na kuwasisitiza mabalozi hao kuhakikisha wanaitumia fursa hiyo kuitangaza Zanzibar kiutalii katika nchi wanazokwenda.

Pia alisema mbali na utalii, ni vyema kuitangaza Zanzibar katika sekta za uchumi wa buluu zikiwamo uvuvi, mafuta na gesi asilia, uvuvi, kilimo cha mwani na bandari huku akisisitiza kwamba iwapo bahari itatumiwa vizuri maendeleo makubwa yatapatikana.

Dk. Mwinyi alisema Dira ya Uchumi wa Buluu inaweza kufanya kazi kwa nchi zote wanazokwenda kuiwakilisha Tanzania, hivyo akasisitiza haja ya kuwakaribisha wawekezaji kuwekeza katika maeneo kadhaa ya viwanda nchini.

Sambamba na hayo, Dk. Miwnyi alisisitiza kwamba kwa upande wa Comoro ni vyema hatua za kurejesha uhusiano na ushirikiano wa kibiashara ukafufuliwa kati ya nchi hiyo na Zanzibar.

Pia alieleza haja ya kuimarisha uhusiano na ushirikiano na Brazil hasa ikizingatiwa kwamba nchi hiyo imepiga hatua kubwa katika sekta ya teknolojia, hivyo ni vyema wakawakaribisha wawekezaji kutoka nchi hiyo kuwekeza nchini badala ya kuagiza bidhaa kadhaa kutoka nchini humo.

Rais Dk. Mwinyi alieleza haja ya kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano ili kuimarisha sekta ya biashara na Kuwait sambamba na kutafuta namna ya kupeleka bidhaa mbalimbali nchini humo zinazotoka Tanzania.

Dk. Mwinyi alisema Urusi ni mdau mkubwa wa utalii nchini hivyo, ni vyema juhudi za makusudi zikaendelezwa kuhakikisha watalii wanakuja nchini sambamba na kuwakaribisha wawekezaji kuwekeza katika maeneo ya utalii.

Awali, Rais Dk. Mwinyi alikutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), ukiongozwa na Mwakilishi Mkaazi, Christine Musisi.

Katika mazungumzo hayo UNDP imekubali kutuma timu ya wataalamu ili kushirikiana na wataalamu walioko serikalini, ikiwa ni hatua ya kupata njia bora ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo kupitia sekta mbalimbali, ikiwamo uchumi wa buluu, kwa lengo la kupata mafanikio.

HABARI KITAIFA

# Wadau watoa maoni kauli ya Samia

**Na Christina Mwakangale**

BAADHI ya wachambuzi na wadau wa siasa, wametoa maoni kuhusu kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, huku wakisema inaonyesha msimamo thabiti na kwamba ana mamlaka hayo. Hata hivyo, baadhi wameshauri kwamba ni wakati wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kukutana na kujadiliana kuhusu suala la Spika Job Ndugai, kuhusu kauli yake ya mikopo.

Juzi Rais Samia alisema kuna baadhi ya watu wamekuwa wakijipanga kwa ajili ya mbio za urais mwaka 2025 na kusahau utekelezaji wa majukumu yao, hivyo anakusudia kuwaondoa ili wakaendelee na harakati zao. Pia alisema hata kauli za baadhi ya viongozi zinatokana na joto la urais 2025.

Wakizungumza jana na Nipashe kwa nyakati tofauti, wachambuzi hao walisema kuna uhusiano mkubwa kati ya chama na serikali na kwamba kutofautiana kimantiki ndani ya chama kikubwa ni kawaida ingawa huhatarisha afya ya kisiasa, hususan utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa.

Abbas Mwalimu, mchambuzi wa masuala ya kisiasa, alisema kauli aliyoitoa Rais juzi, inatokana na mamlaka aliyo nayo na taasisi anayoiendesha, Ikulu, inayobeba masuala yote ya kiutendaji na utekelezaji wa dira na mipango ya maendeleo ya taifa.

"Ikulu ni taasisi iliyo na jukumu la kubeba maono ya kiongozi aliyepo. Maono ya Rais Samia ndiyo ya taasisi ya sasa inayotekeleza mpango wa maendeleo na dira ya taifa. Ibara ya 33 ya Katiba inampa mamlaka ya kuamuru, Rais ni Mkuu wa nchi na Amiri Jeshi Mkuu, anatoa amri.

"Ili kufikia ustawi wa wananchi, unahitajika uratibu, sera zitekelezeke na zinaundiwa sheria, huko bungeni. Kama kuna changamoto hapo maana yake kuna tatizo," alisema Mwalimu.

Naye, mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Gwandumi Mwakatobe, alisema ili kulinda afya ya chama (CCM), ambacho anakitaja ni kikubwa na maarufu barani Afrika, suala la kutofautiana kimsimamo ni la kawaida.

"Ni kawaida chama kikubwa kuwa na mitazamo tofauti na pengine hili lilitegemewa kama alivyosema Rais kwamba ni homa ya uchaguzi 2025. Ingawa ninafikiri ni wale ambao walikuwa wakijiandaa na urais kabla hata ya yeye kuingia mamlakani, bado wana ari hiyo. "Tatizo la Ndugai si hoja yake, yeye ndiye anapitisha fedha bungeni. Tozo amepitisha bungeni leo anasema mikopo haifai. Hajatoa njia ambayo nchi ili ijitegemee ifanye nini. Yeye angezungumza na mhimili mwingine kupata maoni kabla ya kuzungumzia mikopo," alisema Gwandumi.

Juzi, rais Samia alisema atafanya mabadiliko hivi karibuni katika nafasi mbalimbali ndani ya serikali yake, ikiwamo baraza la mawaziri, ili kuondoa waliojiingiza kwenye makundi ya kuwania urais mwaka 2025, ili apate nafasi ya kuwateua watu watakaomsaidia katika kuiongoza serikali kuwatumikia Watanzania.

Alisema safu za uongozi ndani ya CCM, zikiwamo za ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) na wenyeviti wa ngazi mbalimbali, zimeanza kuandaliwa lengo likiwa kujipanga kwa ajili ya urais.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akizungumza na wafanyakazi wa ofisi hiyo kwenye mkutano uliofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Presha, kihoro vyapanda vigogo kusudio Rais kufanya mabadiliko

**Na Mwandishi Wetu**

NI presha na kihoro kwa vigogo ndani ya serikali. Hivyo ndivyo inavyoweza kuelezwa au kubainishwa kutokana na Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza kuwa atafanya mabadiliko ya safu ya uongozi ndani ya serikali yake.

Miongoni mwa maeneo ambayo yanaonekana kufanyiwa mabadiliko ni pamoja na Baraza la Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu wa Wizara na Makatibu Tawala wa Mikoa.

Tangu alipotangaza juzi kuwa atafanya mabadiliko ndani ya serikali, tayari hofu, wasiwasi, shaka na kihoro miongoni mwa walioko kwenye nafasi hizo vimeanza kutawala. Yote hiyo ni kwa sababu hawajui kama wataendelea kuwamo katika nafasi walizo nazo, kuhamishwa au kuachwa kabisa.

Wasiwasi zaidi unaongezeka baada ya kusema atafanya mabadiliko hayo hivi karibuni. Sasa hoja ya kujiuliza ni je, watu watafika wikiendi wakiwa bado hawajatikiswa? au watasherehekea miaka 58 ya Mapinduzi Zanzibar Januari 12, mwaka huu, Rais akiwa ameshatimiza kusudio lake hilo?

Rais Samia alisema atafanya mabadiliko hayo sababu kubwa ikiwa kuwaengua wale ambao wamejiingiza kwenye makundi ya urais 2025 na kuwapa nafasi kuendelea na mbio zao badala ya kuharibu utendaji kazi wa kuwatumikia Watanzania.

Kwa muda mrefu kumekuwa na habari za baadhi ya vigogo wakiwamo mawaziri, kutengeneza makundi kwa ajili ya kuwania urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Habari hizo zilikuwa zikivuma ndani kwa ndani hadi Rais Samia alipopasua jipu kwamba kuna watu wa namna hiyo, miongoni mwao wakiwamo katika timu yake ya uongozi.

Aliweka bayana kwamba aliwateua watu hao katika nafasi hizo, kwa maana ya mawaziri, wakuu wa mikoa na makatibu wakuu wa wizara ili wamsaidie katika kutekeleza miradi ya maendeleo kulingana na sekta wanazoziongoza lakini wamekuwa wakitumia kama fursa kujipanga kwa urais katika uchaguzi ujao.

"Baadhi ya mawaziri na viongozi wa Chama Cha Mapundizi wameanza kujipanga kwa ajili ya 2025, badala ya kujikita kwenye maendeleo ya Watanzania... Nimekaa ni mwezi wa nane sasa nilisema nilikuwa nawasoma nanyi mnanisoma na siku niliyofanya mabadiliko madogo, nilisema hapa nimeweka nukta inaendelea, nataka niwaambie nitatoa 'list' (orodha) karibuni," alisema.

"Wale wote ninaohisi wanaweza kwenda na mimi kwenye kazi ya maendeleo ya Watanzania nitakwenda nao, lakini wale wote ninaohisi ndoto zao ni kule (urais), wanafanya kazi kwa ajili ya kule, nitawapa nafasi waende wakajitayarishe vizuri huko nje kwa sababu nikiwatuma wakiwa ndani itawasumbua, bora niwape nafasi wakajitayarishe tukutane huko mbele ya safari," aliongeza.

Iwapo mabadiliko hayo yatafanyika, yatakuwa ya tatu tangu alipoapa kuwa Rais Machi 19, 2021 baada ya aliyekuwa Rais, hayati John Magufuli, kufariki dunia.

**MABADILIKO YA KWANZA**

Machi 21, 2021 ikiwa ni siku 12 ya kushika hatamu kuongoza Tanzania, Rais Samia alifanya mabadiliko katika baraza la mawaziri ikiwa ni muda mfupi baada ya kuapishwa kwa Dk. Philip Mpango kuwa Makamu wa Rais. Katika kutangaza mabadiliko hayo alisema: "Zege halilali".

Katika mabadiliko hayo alimteua Balozi Liberata Mulamula kuwa mbunge na Waziri wa mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Pia alimteua Balozi Hussein Kattanga kuwa Katibu Mkuu Kiongozi kuchukua nafasi ya Balozi Dk. Bashiru Ally aliyeteuliwa kuwa mbunge.

Walioteuliwa wakati huo ni Dk. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri wa Fedha kuchukua nafasi ya Dk. Mpango na Prof. Palamagamba Kabudi kuwa Waziri wa Sheria na Katiba kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kabla, Mwigulu alikuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mawaziri waliobadilishiwa wizara zao ni pamoja na Waziri Ummy Mwalimu aliyekuwa Muungano na Mazingira kwenda Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na aliyekuwa kwenye wizara hiyo, Selemani Jafo kwenda Ofisi ya Makamu wa Rais.

Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora aliteuliwa Mohamed Mchengerwa huku aliyekuwa akishika nafasi hiyo, George Mkuchika, akiteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi Maalumu.

Hata hivyo, Rais Samia alisema ameona afanye mabadiliko hayo kwa kuwa ni muda mfupi kufahamu nani kashindwa na nani amefanya vizuri katika eneo lake.

**MTIKISIKO SEPTEMBA**

Rais alifanya mabadiliko mengine Septemba 12, 2021 ambayo yalionekana kuleta mtikisiko baada ya baadhi ya mawaziri waliokuwa wameng'ara katika serikali ya mtangulizi wake, ambayo yeye alikuwa Makamu wa Rais, kuondolewa.

Baadhi ya mawaziri walioondolewa ni Dk. Medard Kalemani (Nishati), Dk. Faustine Ndugulile (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) na Dk. Leonard Chamuriho aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

Kutokana na kuondolewa kwa vigogo hao, aliwateua January Makamba (Nishati), Dk. Ashatu Kijaji (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) na Profesa Mbarawa Makame Mnyaa kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Pia alimteua Dk. Stergomena Tax kuwa Mbunge na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, akichukua nafasi ya Elias Kwandikwa, aliyefariki dunia.

# TANESCO yarudisha gharama za awali kuunganisha umeme

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limerudisha gharama za awali za kuunganisha huduma ya umeme kwa wateja wake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ofisi ya Uhusiano ya TANESCO, gharama hizo zilianza kutumika jana.

TANESCO imetangaza kurudisha gharama hizo ikiwa ni siku moja baada Rais Samia Suluhu Hassan kumuagiza Waziri wa Nishati, January Makamba, kuangalia namna ya kuweka viwango vinavyoendana na gharama za kuunganisha huduma hiyo kwa wateja wake.

Rais Samia alisema gharama iliyokuwa imewekwa awali ilikuwa inachangia kulikwamisha shirika hilo kutekeleza majukumu yake ipasavyo ya kuwafikishia wananchi umeme na kuagiza kwamba ni vyema wakaweka viwango ambavyo sio vya juu sana, lakini vya kati ambavyo wananchi watavimudu na pia ambavyo havitalikwamisha shirika.

Shirika hilo lilisema gharama hizo zitakuwa zinatolewa kama ilivyotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA), kupitia gazeti la serikali, taarifa namba 1020 iliyochapishwa Desemba 4, mwaka jana na zimejumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Pia, lilisema kwamba gharama hizo ziliidhinishwa rasmi na EWURA tangu Novemba 25, mwaka jana, baada ya kupitia mchakato wa tathmini wa bei kulingana na gharama halisi ya vifaa vya uunganishaji umeme na kwamba kwa sasa litaondoa kero ya kushindwa kuwafungia huduma ya umeme wateja wake kwa wakati.

Kwa mujibu wa TANESCO, gharama za kuunganisha umeme mjini ndani ya mita 30 kwa mteja wa njia moja kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 320,960, kwa mteja wa njia moja ndani ya mita 70 kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 515,618.

Aidha, umbali wa njia moja ndani ya mita 120 kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 696,670.

Pia, gharama za kuunganisha umeme mjini ndani ya mita 30 kwa mteja wa njia tatu kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 912,014, kwa mteja wa njia tatu ndani ya mita 70 kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 1,249,385, umbali wa njia tatu ndani ya mita 120 kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 1,639,156.

TANESCO walisema gharama ya kuunganisha umeme vijijini kwa wateja wa njia moja ni Sh. 27,000 kama ilivyoelekezwa na EWURA.

Liliwataka wateja waliokwisha lipia Sh. 27,000 kwa ajili ya kuunganishiwa huduma hiyo, kufika katika ofisi za TANESCO, na kwamba lengo la maboresho hayo ni kuliwezesha shirika kuhudumia wateja wengi zaidi.



Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), John Chikomo (katikati), akizungumza na mmoja wa mafundi wanaojenga darasa katika Shule ya Sekondari Burunge kupitia fedha za Maendeleo na Ustawi wa Taifa dhidi ya mapambano ya COVID-19 Wilaya ya Babati mkoani Manyara. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

## Maelfu waripotiwa kuugua kisukari

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WATU 4,396 kisiwani Pemba wameripotiwa kuugua ugonjwa wa sukari kwa mwaka 2020 na mwaka 2021.

Kati ya wagonjwa hao, wanaume ni 1,452 na wanawake ni 2,944 na kwamba mwaka 2020 wagonjwa walioripotiwa ni 1,883 na mwaka 2021 ni 2,513.

Mratibu wa Maradhi Yasioambukiza Pemba, Dk. Yussuf Hamad Iddi, alisema jana kuwa mwaka 2020 katika mkoa wa Kaskazini Pemba, walipokea wagonjwa 1,193 na Kusini wagonjwa 696.

Alisema mwaka 2021 Mkoa wa Kaskazini Pemba walipokea wagonjwa 1,343 na Kusini Pemba wagonjwa 1,170.

Dk. Yussuf alisema mwaka 2021 idadi ya wagonjwa iliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2020 kutokana na wananchi kupima afya zao kwa wingi.

"Mwaka 2020 wananchi walikuwa hawaendi hospitalini kupima afya zao kwani walikuwa wanahofia kuambiwa wana ugonjwa wa corona. Lakini mwaka 2021 walikuwa wanakuja kwa wingi na ndipo tukagundua wagonjwa wengi," alisema.

Pia alisema kati ya wagonjwa walioripotiwa, idadi ya wanawake imekuwa kubwa ikilinganishwa na wanaume kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutokufanya mazoezi.

"Kati ya wagonjwa hao 4,396, wanawake ni 2,944 na wanaume 1,452 ambapo mwaka 2020 wanawake ni 1,883 na wanaume ni 650 na mwaka 2021 wanawake ni 1,711 na wanaume 802", alisema Dk. Yussuf.

Aliwataka watu kufanya mazoezi kila siku kwa muda wa nusu saa kwa kuwa yanajenga afya na huepusha magonjwa mbalimbali yakiwamo ya kisukari.

"Jamii ielewe kwamba mazoezi na kufanya kazi ni vitu viwili tofauti kwa sababu wengine wakimaliza kufanya kazi wanasema wameshafanya mazoezi, hivyo waache dhana hiyo," alisema.

Watu wanaougua magonjwa yasioambukiza wamekuwa wakiongezeka siku hadi siku, huku serikali ikipigania kuondosha magonjwa hayo ili kuwa na taifa lenye afya bora.

# LATRA yaingilia kero usafiri mikoa Kaskazini kwenda Dar

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

KUTOKANA na abiria wanaoelekea Dar es Salaam kutoka mikoa ya Kanda ya Kaskazini kuongezeka, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA), imetoa kibali kwa magari yaliyofungwa vidhibiti mwendo kusafirisha abiria.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Mfawidhi wa LATRA, Mkoa wa Arusha, Amani Mwakalebela, alisema wamefungua milango ya mabasi yote yaliyofungwa vidhibiti mwendo ikiwamo Costal kuchukua kibali cha kusafirisha abiria kwenda Dar es Salaam.

"Mikakati ya LATRA baada ya kuona uhaba wa mabasi yaendayo Dar es Salaam tumefungua milango kwa wamiliki wa mabasi kuja kuchukua vibali, wapeleke abiria," alisema Mwakalebela.

Aidha, aliwataka madereva na watumiaji wa barabara kuendelea kufuata utaratibu na sheria zilizowekwa, ili kuepuka ajali na majanga yoyote yanayoweza kutokea barabarani.

Naye Wakala wa Mabasi yaendayo Dar es Salaam, Emanuel Msagati, alisema hadi kufikia majira ya saa moja asubuhi jana hakukuwa na basi hata moja linaloenda jijini huko.

"Ni kweli abiria ni wengi kiasi cha mabasi kutokutosheleza hivyo abiria wengine walilazimika kughairi safari zao na kujipanga kwa kesho, wengi waliofanikiwa kusafiri ni waliokata tiketi juzi," alisema Msagati.

Happiness Laban ni mmoja wa abiria aliyeahirisha safari baada ya kukosa usafiri, alisema alifika saa 12: 30 asubuhi lakini alikuta gari zimejaa.

"Nilifika hapa saa 12: 30 asubuhi nikijua nitapata usafiri kama kawaida lakini ikashindikana na bahati mbaya sikukata tiketi nikijua nitabahatisha usafiri asubuhi, nimekaa kituoni hadi muda huu nikijua pengine yatakuja yale mabasi ya saa tano lakini nimekata tamaa na nimeamua kukaa hapa nipumzishe akili na nimekata tiketi tayari kwa ajili ya kesho," alisema Labani.

HABARI KITAIFA

# Miaka mitano jela kuua shemeji bila kukusudia

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala ya Sumbawanga imemtia hatiani na kumhukumu kifungo cha miaka mitano jela David John, maarufu Silwela kwa kumuua bila kukusudia shemeji yake, Alex Simwanza.

Mahakama hiyo mbele ya Jaji Dustan Ndunguru, kabla ya kumtia hatiani ilimuona mshtakiwa kutenda kosa la mauaji ya bila kukusudia badala ya kosa la mauaji ya kukusudia aliloshtakiwa nalo awali.

Upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi saba na wa utetezi, mshtakiwa alijitetea kwa kupinga kufanya mauaji hayo.

Mahakama kabla ya kutoa hukumu ilisikiliza maoni ya wazee wa baraza na Edina Kaisile katika kuchambua ushahidi wa pande zote mbili kwa maoni yake aliona kwamba mshtakiwa hakuua kwa kukusudia bali aliua bila kukusudia, lakini maoni yake yalitofautiana na wazee wengine wa baraza.

Wazee wengine wawili Salome Kapele na Jelas Simchindo kwa pamoja waliona mshtakiwa hakutenda kosa hilo la mauaji.

Jaji Dustan Ndunguru alisema kutokana na mazingira ya kifo cha Simwanza, mshtakiwa ameua bila kukusudia chini ya kifungu cha sheria ya kanuni ya adhabu namba 195 na mahakama inamtia hatiani kwa kosa hilo. Baada ya kutiwa hatiani upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Peres Simon, ulidai mshtakiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza amesababisha kifo ndani ya familia anaomba apewe adhabu kwa mujibu wa sheria ili iwe funzo kwake na watu wengine.

Wakili wa utetezi, Neema Charles aliomba mshtakiwa asipewe adhabu kali, kwa madai alishambuliwa na shemeji zake kwa kumpiga na yeye alikuwa anajitetea.

Alidai mshtakiwa ni kijana mdogo mwenye umri wa miaka 23 na amekaa rumande miaka miwili na miezi saba, anategemewa na familia, na kuomba apewe adhabu ndogo.

"Kwa mazingira yaliyozunguka tukio imeonyesha kwamba mshtakiwa na marehemu ni mtu na shemeji yake, mahakama inampa adhabu ya kifungo cha miaka mitano jela kwa kosa la kuua bila kukusudia," alisema Jaji Ndunguru.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa anadaiwa alitenda kosa hilo Mei 14, 2019, maeneo ya Kisisiwe Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa.

Mshtakiwa alikana na taarifa ya uchunguzi wa daktari ilionyesha marehemu alipigwa na kitu kilichosababisha kuvuja kwa damu katika ubongo. Mashahidi upande wa mashtaka walikuwa saba na shahidi wa tano Issack Mwakasege, alidai kwamba Mei 14, mwaka 2019, jioni alikuwa anatokea Mbeya kwenda Sumbawanga alipigiwa simu na Katibu wa mtaa Alex Masumbulio, akimweleza kwamba nyumbani kwa Simwanza kuna ugomvi kati ya David na shemeji zake Alex na Aidan, akamtaka akatoe taarifa polisi.

Baada ya dakika 20 Katibu akampigia simu tena na kumweleza kwamba Alex na Fredrickson Alex, wakati wanakwenda kuripoti polisi walishambuliwa wakaanguka na pikipiki, asubuhi ya Mei 15, aliambiwa Alex amefariki.

Alipofika nyumbani aliwakuta ndugu zake, lakini mama yake alimfahamisha kuwa David alimshambulia wakati anasuluhisha ugomvi kati ya David na mkewe Pendo, wakati huo Pendo alikuwa ndani ya uzio lakini David alikuwa nje ya uzio.

Ilidaiwa David aliingia ndani na kupinga maelezo yaliyokuwa yakitolewa na mama mkwe wake, mabishano yaliendelea na alitaka kumshambulia mama lakini alizuiliwa na kina Alex.

Pia, ilidaiwa David alipasua vioo vya pembeni vya pikipiki, baada ya tukio hilo Alex na Fredrick walikwenda kutoa taarifa Kituo cha Polisi Sumbawanga na wakati wakiwa njiani maeneo ya shamba la mkonge David alimvamia Alex alipoanguka akaanza kumpiga.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akizungumza na wananchi baada ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Sebleni Jimbo la Kwahani unaotekelezwa kupitia fedha za mfuko wa jimbo. **ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jafo asisitiza ufanisi katika miradi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amesema serikali ya Muungano na ile ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zimedhamiria kuhakikisha miradi yote inatekelezwa kwa ufanisi.

Dk. Jafo alisema hayo juzi wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua na kuzindua miradi ya majisafi na salama katika majimbo ya Chumbuni na Amani pamoja ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Sebleni Jimbo la Kwahani, inayotekelezwa kupitia Fedha za Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF), Zanzibar.

Akizungumza kwa nyakati tofauti akiwa kwenye ziara hiyo, alisema kupitia usimamizi thabiti wa watendaji, serikali zote mbili zitahakikisha miradi hiyo inakamilika kwa viwango na ufanisi mkubwa.

Pia waziri huyo aliwapongeza wataalamu wanaosimamia miradi hiyo kwa kusema kuwa anafarijika kuona matumizi ya fedha yanaendana na ubora na viwango.

"Leo hii hata ukisema miradi haitekelezeki, mimi nasema hapana maana nimefika hapa na kwa macho yangu nimejionea mwenyewe miradi hii iko vizuri naomba niwapongeze sana kwa kuisimamia vyema na kuitekeleza kwa wakati," alisema.

Waziri Jafo aliongeza kwa kusema kuwa kukamilika kwa miradi hiyo ya CDCF kutaweza kutoa fursa na kuwanufaisha wananchi pamoja na kubadilisha maisha yao kwa ujumla.

Awali, akizungumza katika mkutano huo na wananchi wa Shehia ya Banko katika Wilaya ya Magharibi, Rashid Simai Msaraka, alisema aliahidi kuwa wataendelea kuhakikisha fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo zinatumika kama ilivyopangwa.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Amani, Mussa Hassan Mussa alipongeza juhudi za serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo huku akiwataka kutoiharibu ili iendelee kuwanufaisha.

## Wafugaji watakiwa kufuga kibiashara

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka wafugaji nchini kufuga kibiashara na kuachana na ufugaji wa kuchunga ambao tija yake imekuwa ndogo kwao na kwa taifa pia.

Ndaki alitoa rai hiyo jana alipotembelea shamba la kisasa la mifugo la Shaffer, mkoani hapa.

Akiwa katika shamba hilo akikagua shughuli mbalimbali zinazoendelea kwenye eneo hilo, alisema wanawashauri wafugaji kuanza kufuga kisasa na kuachana na ufugaji wa kiasili ambao sasa umeanza kupitwa na wakati.

"Tumekuwa hatuoni faida kwa mifugo yetu kwa sababu ya kung'a ng'ania ufugaji wa kiasili, wafugaji tuanze kufuga kibiashara ili tuongeze tija ya mifugo yetu," alisema Ndaki. Aliongeza kuwa ili waanze kuona tija ya ufugaji wao ni lazima wabadilike na waache ufugaji wa kuzunguka kutafuta maeneo ya malisho na badala yake wawe na maeneo yao ya kufugia ambayo yatakuwa rahisi kufikiwa na wataalamu kwa ajili ya kuwapatia huduma zinazohitajika kwa mifugo yao.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Bashiru Muhoja, alisema mwekezaji wa shamba la mifugo la Shaffer anauhitaji mkubwa wa chakula cha mifugo kama vile soya na mahindi.

"Mheshimiwa waziri, huyu mfugaji ana uhitaji mkubwa wa soya, mahindi na alfaalfa ambapo kwa sasa vyote anavitoa nchini Zambia. Hii ni fursa kwa wananchi wetu na tumeshaanza kuchukua jitihada na tuna orodha ya wakulima ambao wako tayari kulima mazao hayo kwa ajili ya kumuuzia mfugaji huyu," alisema Muhoja

Msimamizi wa Shamba la Shaffer, Mahboob Malick, alisema wanaishukuru serikali kwa ushirikiano mkubwa inaowapatia na kwamba wako tayari kuendelea kushirikiana nayo kwa lengo la kuboresha ufugaji nchini.

"Sisi tuko tayari kupokea vijana ambao wanataka kujifunza ufugaji. Waje hapa tutawafundisha namna bora ya ufugaji wa kisasa ili wakipata ujuzi huu waende kuwafundisha na wenzao na hatimaye kuboresha ufugaji wetu," alisema Malick.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kushuka bei ya mafuta kulete nafuu

**JANA** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilitangaza bei mpya za petroli, ambayo imeshuka kati ya Sh. 4 hadi 35 na dizeli Sh. 43 hadi 67 kwa Bandari ya Dar es Salaam.

Bei hizo zinashuka kutoka Sh. 2,510 kwa lita moja ya petroli ambayo sasa itauzwa Sh. 2,501, huku bei ya dizeli kupungua kutoka Sh. 2,325 hadi 2,234.

Kwa Bandari ya Tanga bei ya petroli itashuka kutoka Sh. 2,521 hadi 2,525, huku Bandari ya Mtwara kutoka 2,569 hadi 2,534.

Kwa upande wa bei ya dizeli kwa Tanga itapungua kutoka Sh. 2,413 hadi 2,369, Bandari ya Mtwara ikiwa ni kutoka Sh. 2,423 hadi 2,425 huku bei ya mafuta ya taa ikipanda kwa Sh. 99.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Godfrey Chibulunje, alisema bei za mafuta zingepungua zaidi iwapo thamani ya Dola za Marekani isingeongezeka dhidi ya Shilingi ya Tanzania.

Kwa sasa Dola ya Marekani inanunuliwa kwa Sh. 2,314.23 ikiwa ni ongezeko la asilimia moja kutoka Sh. 2,300.88, huku tozo za taasisi za serikali zilizopunguzwa Oktoba mwaka jana zilisaidia kupunguza bei ya mafuta kwa kati ya Sh. 23 na 31 kwa lita kutegemeana na aina ya mafuta.

Kushuka kwa bei hizi ni habari njema kwa Watanzania kwa kuwa mafuta yalisababisha mfumuko wa bei kwenye bidhaa nyingi kiasi cha wengi kushindwa kumudu.

Kwa sasa bei za vyakula na bidhaa nyingine zimepanda na zilikuwa zinaendelea kupanda na sababu kubwa inayotajwa ni kupanda kwa bei ya mafuta, sasa imeshuka tunatarajia kuona mabadiliko kwenye bei hizo.

Kwenye ujenzi kinachoelezwa kupanda kila siku ni chuma kiasi cha nondo ya milimita 12 iliyokuwa inauzwa Sh. 19,000 mwaka jana, sasa inauzwa Sh. 27,000 ikiwa ni ongezeko la Sh. 7,000 kwa moja, haya ni maumivu makubwa kwa wanaojenga sasa.

Mafuta ya kupikia ya alizeti lita tano yamefika Sh. 36,000 huku lita moja ikiuzwa Sh. 9,000, hali hii sio nzuri kwa sababu hata bidhaa za sokoni kama maharagwe, mahindi, mchele, unga na vinginevyo muhimu kwa maisha ya kila siku vimeongezeka bei na wote sababu kubwa ni kupanda kwa gharama za usafiri kutoka shambani hadi sokoni.

Bei zinapopanda anayeumia ni mwananchi wa kawaida kabisa ambaye atajikuta anatumia fedha nyingi huku hali yake ikiendelea kuwa duni, atashindwa kutimiza mahitaji ya msingi kwa kuwa kipato kinakuwa kile kile licha ya ongezeko la gharama.

Lakini ni muhimu mamlaka za serikali kufuatilia bei za bidhaa mbalimbali hasa za vyakula na ujenzi ambazo kila uchao zinazidi kupaa na wanaoumia ni wengi kwa kuwa ni lazima watu wale.

Tunaamini kushuka kwa bei za mafuta kutaonyesha ahueni kwa wananchi na lazima kuwe na ufuatiliaji wa karibu kwa kuwa wengi wanalangua bidhaa ili kujipatia faida, lakini wanaoumia ni wananchi, kwamba kuanzia wasafirishaji washushe gharama za usafiri ili wauzaji wa bidhaa wafanye hivyo.

Ufuatiliaji wa karibu utasaidia kuwatambua walanguzi ili kuchukua hatua madhubuti mapema, kwa kuwa lengo ni kumwezesha mwananchi wa kawaida kumudu maisha yake huku akiendelea kulipa kodi.

Tayari wananchi wamebanwa kwenye tozo mbalimbali kwenye kulipia umeme, miamala ya simu, anaponunua mafuta ya petroli na dizeli, pia kwenye bidhaa kuna kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), zote hizi ni mzigo kwa mwananchi hivyo ni lazima tuone ahueni kwake ili gharama za maisha zishuke.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hivi ndivyo kulivyo penye vinara chanjo UVIKO-19

Na Sabato Kasika

**CHANJO** ya UVIKO-19 iliyozinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa mwezi Julai mwaka jana. Tunaelezwa kwamba, hadi kufikia Desemba 18, mwaka jana, ambayo ni wiki mbili na nusu iliyopita, kuna watu milioni 1.27 waliokwishapata chanjo kamili ya kujikinga na ugonjwa huo.

Katika jitihada za kuhakikisha Watanzania wanapata huduma hiyo, mikoa mitano inatajwa kuongoza kwa kufanya vizuri kwa utoaji chanjo hiyo, ambayo ni Mwanza, Ruvuma, Mara, Kagera na Dodoma.

Inapoenda kinyume chake, ni kwamba wananchi wa mikoa mingine mitano ya Manyara, Songwe, Njombe, Singida na Iringa wanadaiwa kufanya vibaya katika utoaji chanjo hiyo. Tanzania Bara ina mikoa 26 ambayo mikoa 10 kati ya hiyo, taarifa zake zimejulikana kuhusu jinsi inavyotoa chanjo, lakini bado kuna mingine 16 ambayo wizara yenye dhamana ya afya za Watanzania haikutajwa

Pamoja na hayo, ni wazi kwamba kuna haja kwa mikoa 21 ikiwamo inayodaiwa kufanya vibaya, inajifunza kitu kutoka mitano ambayo wizara inaitaja kuwa imefanya vizuri katika utoaji chanjo.

Kujifunza kutoka kwa wengine, kunaweza kugeuza makosa kuwa mafanikio. Hivyo, si vibaya mikoa ambayo bado inasuasua katika chanjo, inajifunza kutoka zile ambazo zimepiga hatua katika utoaji chanjo hiyo.

Ikumbukwe, ili kuwa mshindi ni muhimu kujifunza kutokana na makosa, kwani bila ya kufanya hivyo, mtu anaweza kujikuta akiendelea kukosea tu au kushindwa kupiga hatua kwenda mbele.

Mikoa kusuasua katika utoaji chanjo, ni wazi kuna sababu mbalimbali zinazochangia kusaidia kujirekebisha, hasa kujifunza kwa mikoa, ambayo imepiga hatua ili kujua mbinu zilizotumika.

Kama kuna jambo watu hawalipendi, jamii kuambiwa wamekosea. Wengi wanatamani waishi bila ya kufanya makosa, lakini hilo haliwezekani. Ndiyo maana, kuna suala la kujifunza kutokana na makosa. Ndani ya mazingira ya duniani, hakuna namna ambayo mtu anaweza kuishi bila ya kufanya makosa. Watu wanakosea kila siku inayoenda kwa Mungu, wakijua hata wakati mwingine kwa kutojua wamekosea. Hivyo, umuhimu wa kujifunza kutokana na makosa una uzito wake, hata kwenye suala la chanjo, inamaanisha kwamba mikoa iliyoko nyuma katika utoaji chanjo, ijifunze mahali ilikokosea, ili zichukue hatua za kujirekebisha.

Taarifa za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, zinaonyesha tangu chanjo ya UVIKO-19 ilipozinduliwa mwishoni mwa Julai hadi kufikia Desemba 18, mwaka jana, kuna watu milioni 1.27 waliokwishapata chanjo hiyo.

Wizara pia imesema, kuwa taarifa potofu kuhusu chanjo hiyo inachangia baadhi ya watu kukana kuchanjwa. Hivyo, ni vyema viongozi wa mikoa wakaliona hilo linakwamisha chanjo katika maeneo yao, walifanyie kazi.

Hatua hiyo ya kuangalia vikwazo vya chanjo, ingeenda sambamba na kuhimiza watu kuzingatia mwongozo wa kudhibiti ugonjwa huo, kwani wengine wanaonekana kutochukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa Uviko - 19.

Mwongozo wa sasa unataka watu waepuke hali ya mikusanyiko isiyo ya lazima, pia kunahitajika watu wavae barakoa, kunawa maji tiririka na kutumia vitakasa mikono na penye usafiri abiria wa umma, idadi ya abiria ifanane na viti kwenye basi.

Ukweli ni kwamba, penye baadhi ya maeneo, ni kama watu hawana habari na ugonjwa huo hawachukui hatua za kujikinga, hali inayokaribisha ujio wa UVIKO -19 kuendelea kuwapo nchini.

Iwapo watu hawatazingatia mwongozo huo, ni wazi watashindwa kujitokeza kupata chanjo. Hivyo, si vibaya viongozi wa mikoa iliyo nyuma katika chanjo, wakaenda kujifunza kwa wenzao ambao mikoa yao iinaoongoza.

Wizara yenye dhamana na afya inatukumbusha kuwa, hali ya maambukizi ya UVIKO imeongezeka, jambo ambalo si ishara nzuri kijamii. Watanzania wanatakiwa kuchukua tahadhari zinazoelekezwa na wataalamu wa afya, ili wabaki salama dhidi ya ugonjwa huo.

Ni katika uthibitisho sasa, wizara hiyo inasema idadi ya sampuli nyingi zinazopokewa katika Maabara Kuu ya Taifa, zimekuwa zikiongezeka kutoka siku 14 hadi kufikia 47, hali inayoashiria ongezeko la maambukizi hayo.

## Serikali yaondoa waishio hifadhini

**Na Amon Mtega,** NAMTUMBO

WAKAZI wa Kijiji cha Mtumbatimaji, Kata ya Mgombasi wanaofanya shughuli za kilimo katika eneo la Kihindambue, wameanza kuondolewa kupisha uhifadhi katika Mlima wa Linole, Matogoro 'B'.

Wakizungumza jana kwa nyakati tofauti, Twaliki Mbilo, amesema eneo hilo walipewa na Serikali ya Kijiji cha Mtumbatimaji tangu mwaka 2014 na kushangaa kuambiwa wahame kuwa ni hifadhi ya maliasili.

Mbilo alisema wanahamishwa kwa nguvu na yeye kuezuliwa nyumba huku mahindi aliyokuwa ameyahifadhi yakibebwa pamoja na mifugo na kuiomba serikali kuwaachia eneo hilo kwa madai kuwa ndiyo sehemu wanayojipatia riziki.

Kwa upande wake, Athumani Mapunda amedai nyumba yake kuchomwa moto na mbuzi 16 kuchukuliwa.

Kutokana na sakata hilo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mtumbatimaji, Liwanda Makunjalila, alisema mikutano ya makubaliano ya kuwahamisha wanaofanya shughuli za kibinadamu katika eneo hilo ilifanyika na walifikia makubaliano mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Dk. Julius Ningu.

Alisema kutokana na mkutano huo uliofanyika chini ya mkuu wa wilaya, yalifikia makubaliano ya kuwatambua wakazi wote wanaofanya shughuli za kibinadamu katika eneo hilo na ofisi ya kijiji ilifanya, na taarifa hizo zimepelekwa katika ofisi ya mkuu wa wilaya.

Dk. Ningu kwa upande wake alisema kuwa eneo hilo la milima wa Linole ni Hifadhi ya Milima Matogoro 'B' na makubaliano wananchi wanatakiwa kuliachia ili shughuli za uhifadhi wa misitu ziendelee na vyanzo vya maji vilindwe.

Dk. Ningu alisema kabla ya makubaliano hayo mkutano ulifanyika na ofisi yake iliagiza kwenye ofisi ya kijiji kwenda kuwaorodhesha watu wote waliopo kwenye eneo hilo ili kupata takwimu sahihi.

Kuhusu baadhi ya watu wanadaiwa kuezuliwa nyumba na kuchomewa, alisema hilo halijui kwa kuwa hakuna nyumba inayojengwa ndani ya hifadhi.

# Watu 32 wafariki matukio ya moto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATU 32 wamefariki dunia na wengine 145 wamejeruhiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka jana, kutokana na matukio ya moto.

Kutokana na vifo hivyo, chanzo kikuu kimeelezwa kuwa ni uzembe na hitilafu za umeme kwa watu kujiunganisha nishati hiyo.

Taarifa iliyotolewa na Msemaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACF), Puyo Nzalayaimisi, inasema katika kipindi hicho watoto 10 wameripotiwa kutumbukizwa kwenye matundu ya vyoo na mama zao. Akitoa taarifa hiyo jijini hapa jana, SACF Nzalayaimisi alisema katika kipindi hicho, jeshi limekabiliana na zaidi ya matukio ya moto 1,800.

Kuhusu matukio ya baadhi ya kinamama kutumbukia katika matundu ya vyoo, alisema katika kipindi cha mwaka jana, matukio hayo yamezidi kushamiri huku mikoa ya Kanda ya Ziwa ikionekana kuongoza.

Katika hatua nyingine, alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi dhidi ya matukio ya ajali za moto katika maeneo ya masoko nchini huku akibainisha chanzo cha ajali hizo.

Alisema jeshi hilo pia limefanya uokozi mara 694 na kwamba matukio hayo yalisababisha vifo 388 na majeruhi 763 huku akibainisha majanga mengi ya moto yanatokana na uzembe, hujuma na hitilafu za umeme.

Ili kudhibiti na kupunguza matukio hayo, alisema jeshi hilo linaendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali na namna ya kujikinga pale yanapotokea majanga.

Katika kufanya hivyo, kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka jana, walitoa elimu katika maeneo 2,474 na watu 197,183 wamenufaika na elimu hiyo moja kwa moja mbali na ile ya kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Kadhalika, alisema jeshi limefanya ukaguzi wa majengo 19,202 huku serikali ikiendelea kuliwezesha kwa kulipatia vifaa vya kisasa vya kuzimia moto na uokozi.




Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Wenye Ulemavu), Ummy Nderiananga, akimtwisha ndoo ya maji mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Mchanga Mdogo Pemba baada ya kuzindua rasmi kisima cha maji kinachotarajiwa kutatua changamoto shuleni hapo. **PICHA: NYAMAGORY OMARI**

# Taasisi yasaidia waliofungwa kwa kukosa faini kutoka jela

**Na Christina Haule,** MOROGORO

TAASISI ya Ukumbusho wa Zaka Tanzania (TAUZAKTA) Mkoa wa Morogoro, imelipa Sh. 500,000 kwa ajili ya faini na kuwatoa wafungwa walioshindwa kulipa na kusababisha kwenda kutumikia kifungo katika Gereza la Mkoa wa Morogoro.

Mwenyekiti wa TAUZAKTA Mkoa wa Morogoro, Juma Kitunga, alisema jana kuwa wafungwa hao wawili walishtakiwa kwa makosa mbalimbali na kutakiwa kwenda jela au kulipa faini na kukosa hatua ambayo ilisababisha kwenda jela.

"Utakuta mtu kashtakiwa kwa kosa dogo tu na hukumu yake ikaangukia kwenye kifungo au faini ya Sh. 200,000 lakini ana maisha duni, hawezi kumudu gharama hiyo. Anaishia kwenda jela miezi mitatu au sita na sisi tumeanza utaratibu wa kuwasaidia wafungwa hawa," alisema.

Kitunga alisema kwa sasa wanajipanga kuwasiliana na mkuu wa magereza mkoa ili kupata idadi kamili ya wafungwa waliokosa kulipa faini na kuishia kutumikia vifungo magerezani ili waingizwe kwenye maombi kwa nchi zinazotoa zaka za misaada ya kuwakomboa wenye kuhitaji msaada.

Alisema suala la kuwakomboa watu katika vifungo lipo tangu zamani na hata kwenye vitabu vya dini lipo na kwamba watu waliokuwa wakitumikishwa kwenye enzi za utumwa ilifika mahali walikuwa wanakombolewa kwa fedha.

Kwa kutumia hali hiyo na hasa uwepo wa watu wenye mioyo ya kuwakomboa, alisema watu kwenye nchi kama Saudi Arabia wanaweza kutoa fedha za kuwakomboa waliokosa faini na kutumikia vifungo katika magereza.

Naye Katibu wa TAUZAKTA Mkoa wa Morogoro, Kigozi Shabani, alisema wamekuwa wakitoa misaada mbalimbali ya kujikimu kwa mahabusu yenye thamani ya kuanzia Sh. 50,000 hadi 100,000 ambayo alisema bado ni midogo kutokana na kukosa wafadhili wa uhakika.

Tangu taasisi hiyo ianze mwaka 2014, alisema wamekuwa wakiomba pesa kutoka kwa watu binafsi kusaidia mahabusu na wafungwa kwa vitu mbalimbali kama sabuni, miswaki, mafuta na pedi kwa ajili ya kinamama.

Kutokana na jitihada hizo, aliiomba serikali na wadau wa masuala ya kijamii kuiangalia taasisi hiyo kwa jicho la tatu kwa kuwa ina lengo la kusaidia jamii katika makundi mbalimbali.

Wakili wa kujitegemea, Ignas Punge, aliwashauri mawakili wa washtakiwa mbalimbali mahakamani kuangalia mienendo ya kesi za wateja wao na kuwaandaa kujipanga kulipa faini kama kesi ina mwelekeo huo ili kuwaepusha kwenda magerezani ambako wanaweka msongamano usio na maana.

Punge alisema kwa mujibu wa sheria, mshtakiwa akipata hukumu ya faini au kifungo anayo nafasi ya kulipiwa faini muda wowote na kuwa huru.

Aliyataja baadhi ya makosa ambayo mshtakiwa anaweza kupata adhabu ya kifungo au faini kuwa ni makosa ya usalama barabarani, kumtukana mtu au kumjeruhi mtu na kwamba adhabu hizo na nyingine kama hizo kisheria zimewekwa ili kuondoa msongamano magerezani.

# Bodi Mazao yawatoa hofu wananchi akiba ya mahindi

**Na Francis Godwin,**
IRINGA

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imewatoa hofu wananchi kuwa mahindi yako ya kutosha katika hifadhi licha ya kuendelea kuuzwa nje ya nchi.

Pia imesema bei ya zao hilo bado haijapanda kulinganisha na mwaka 2016.

Kwa mwaka 2016, bei ya mahindi kwa Januari ilifikia Sh. 1,050 kwa kilo lakini kwa mwaka huu, bei kwa ujazo huo ni kati ya Sh. 500 na 600, hivyo hali ya chakula bado ni nzuri.

Akizungumza jana kwa niaba ya Meneja wa CPB Nyanda za Juu Kusini, Anganyila Kamihanda, alisema lengo kubwa la taasisi hiyo ni kuendelea kufanya biashara na sasa biashara kubwa ni uuzaji wa mahindi.

“Ikumbukwe hapa katikati hali ya uuzaji wa mahindi ilikuwa mbaya hadi kusababisha hifadhi zetu kujaa ila sasa tumefanikiwa kupunguza akiba kubwa ya mahindi tuliyokuwa nayo kwa kupitia mikataba ya ununuzi wa mahindi tuliyoingia na kampuni za Rwanda na Kenya,” alisema.

Alisema katika kituo cha Iringa walikuwa na hifadhi ya mahindi tani 18,000 kabla ya Rwanda kununua tani 5,000 hivyo akiba ambayo watabaki nayo ni tani 13,000 ambazo wanaendelea kusaga unga na kusambaza ndani ya nchi kwa gharama nafuu zaidi.

Pia alisema kwenye vituo vingine vya Songwe na Songea mkoani Ruvuma, bado wanayo hifadhi ya kutosha na kama hali ya ukame itaendelea, bado hakutakuwa na hofu yoyote kwa kuwa hifadhi iliyopo ni kubwa zaidi. Pia alisema Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) ina akiba ya kutosha.

Alisema ikitokea mahindi yamepungua watakwenda kuchukua mahindi kwenye NFRA ambako kuna akiba ya kutosha.

Kwa kawaida, alisema bei ya mahindi iliyopo ni nzuri na nafuu kwa wananchi kwa kuwa kama ingepanda Septemba au Oktoba, basi ingekuwa mbaya zaidi na hofu ingekuwa kubwa.

Pia alisema licha ya changamoto za mvua zilizokuwapo, bei ya mahindi haitapanda badala yake mwakani wakulima watakuwa na neema zaidi ya bei nzuri ya mazao.



Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, akikata utepe kuzindua madarasa katika Shule ya Sekondari Mataka. PICHA: STEVIE CHINDIYE

## DC apiga ‘stop’ ujenzi makazi eneo la serikali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, amepiga marufuku ujenzi katika eneo la Mitamba ambalo ni la serikali.

Msafiri amewataka watu wote waliovamia na kujenga katika eneo hilo, watakaokaidi agizo lake, watakuwa wanapoteza muda na watachukuliwa hatua.

Akizungumza na baadhi ya wananchi wanaodaiwa kuvamia eneo hilo jana, Mkuu huyo wa Wilaya alikemea kitendo cha watu kuvamia maeneo ya serikali na yenye hati miliki bila kufuata taratibu.

Alisema wako watu wanaotumia nguvu nyingi za kujenga kwenye maeneo yanayomilikiwa kihalali ambao baadaye wakivunjiwa wanarudishwa nyuma kimaendeleo.

“Hakuna hata siku moja serikali itakuja kuwaachia maeneo mlipovamia. Hata kama itaacha, itatoa kwenye mamlaka za upangaji yaani Mkurugenzi wa Halmashauri.

Hapo ni kwamba kama umejenga katika eneo la serikali ni sawa na mtu anayelala nje,” alisema Msafiri.

Mkuu wa Wilaya aliwataka wananchi kuheshimu ardhi za serikali na zinazotambulika kihalali na kuacha tabia ya kuvamia maeneo yasiyo ya haki kwao.

Aliwataka wavamizi kuondoka na kuacha kujenga eneo la Mitamba na kwamba atayekaidi na kuendelea atakuwa anajidanganya kuwa atapata haki au kulipwa au kupewa eneo hilo.

# Watakiwa kupeleka korosho maghala ya ushirika

**NA Stevie Chindiye,**
TUNDURU

WAJUMBE na Wahandisi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) wilayani Tunduru wametakiwa kupeleka korosho zote kwenye maghala ya Chama Kikuu cha Ushirika (TAMCU).

Hatua hiyo ni juhudi za kutunisha mfuko wa chama na kukifanya kupiga hatua kimaendeleo.

Mwenyekiti wa TAMCU, Mussa Manjaule, alitoa maagizo hayo juzi wakati akizungumza na viongozi hao katika mkutano mkuu maalumu uliofanyika katika ukumbi wa Klasta ya Walimu wa Tarafa ya Mlingoti, mjini hapa.

Manjaule alisema kwa kufanya hivyo watajenga uwezo kwa chama chao na kukiwezesha kufanya shughuli za kimaendeleo tofauti na sasa ambapo viongozi wamekuwa wakipeleka korosho katika maghala binafsi na kuwaneemeesha kutokana na nguvu ya wakulima ambao ni wanachama wa ushirika.

Alisema hadi sasa takwimu zinaonyesha kuwa zadi ya tani 1,000 za korosho zilizouzwa katika msimu wa mwaka 2021/22 zilipelekwa katika maghala binafsi huku maghala ya chama yakiwa yamepokea wastani wa tani 600 tu.

Kwa mujibu wa Manjaule, wakati hayo yakiendelea viongozi hao pia wamekuwa ndio walalamikaji wakubwa kwamba chama kikuu kimekuwa hakiwalipi posho pindi wanapowaita kwenye vikao na kwamba kama mtindo ndio huo, TAMCU itawalipa posho kutoka wapi.

Alisema chama kinayo mipango mingi ya kutekeleza ikiwamo utaratibu wa kufungua duka la kuuza pembejeo na viuatilifu kwa wanachama na kuwaondolea kero ya kuuziwa dawa feki au zilizochakachuliwa na kuwaangusha kwenye uzalishaji pamoja na ujenzi wa maghala mapya. Pia alisema mipango hiyo itakifanya chama kujiimarisha kiuchumi na kumudu kusimamia wanachama wake.

Meneja Mkuu wa TAMCU, Imani Kalembo, aliwataka viongozi hao kuwa waaminifu wanapotekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na kurudisha fedha za wakulima ambazo zinaweza kuingia katika vyama vyao kimakosa.

Alisema uzoefu unaonyesha viongozi Mshikamano AMCOS waliingiziwa kwa bahati mbaya Sh. milioni 18 ambazo mwandishi mkuu kwa kushirikiana na bodi ya uongozi walizitoa baada ya kuandika majina ya ndugu zao. Hata hivyo, alisema baada ya kufuatiliwa na kubainika na kutakiwa kuzirejesha kwa kutumia vyombo vya dora, mmoja wa viongozi hao alianza kulalamika kuwa wanaonewa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Mwenyekiti wa Sama AMCOS, Ally Yasini, na Karistu Makolela wa Chichilimbe AMCOS, walisema kilichowakimbiza ni uwapo wa watumishi wa serikali katika ghala hilo ambao hawaelewi taratibu za ushirika.

Pia walisema miongoni mwa mizani iliyopo hapo huwaibia mazao ya wakulima na kusababisha hasara kubwa kwenye vyama vyao tofauti na uzito huo huo kuwa sawa pindi wanapopeleka katika maghala binafsi.

Kutokana na hali hiyo, viongozi hao waliwataka viongozi wa TAMCU kufanya ufuatiliaji na kutatua kero hizo na kwamba wako tayari kuanza kupeleka korosho za wakulima wao ili kusaidia kutunisha mfuko wa chama na si kutunisha matumbo ya watu wachache.

HABARI KITAIFA

## Zaidi ya 4,000 waripotiwa kuugua kisukari

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WATU 4,396 kisiwani Pemba wameripotiwa kuugua ugonjwa wa sukari kwa mwaka 2020 na 2021.

Kati ya wagonjwa hao, wanaume ni 1,452 na wanawake 2,944 kwa mwaka 2020 wagonjwa walioripotiwa ni 1,883 na 2021 ni 2,513.

Akizungunza na mwandishi wa habari hizi, Mratibu wa maradhi yasiyoambukiza Pemba, Dk. Yussuf Hamad Iddi, alisema, mwaka 2020 katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, wamepokea wagonjwa wa kisukari 1,193 na Kusini 696.

Alisema kuwa, mwaka 2021 Mkoa wa Kaskazini Pemba walipokea wagonjwa wa kisukari 1,343 Kusini walipokea wagonjwa 1,170.

Dk. Yussuf alisema, mwaka 2021 idadi ya wagonjwa imeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2020 kutokana na wananchi kupima afya zao kwa wingi.

"Mwaka 2020 wananchi walikuwa hawaendi hospitali kupima afya zao, kwani walikuwa wanahofia kuambiwa wana ugonjwa wa corona, lakini mwaka 2021 walikuwa wanakuja kwa wingi na ndipo tukagundua wagonjwa wengi," alisema mratibu huyo.

Alifafanua kuwa, kati ya wagonjwa hao walioripotiwa, idadi ya wanawake imekuwa kubwa ikilinganishwa na wanaume kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutofanya mazoezi.

"Kati ya wagonjwa hao 4,396, wanawake ni 2,944 na wanaume 1,452, ambapo mwaka 2020 wanawake ni 1,883 na wanaume ni 650 na mwaka 2021 wanawake ni 1,711 na wanaume 802," alisema Dk. Yussuf.

Aliwataka wanajamii wafanye mazoezi kila siku kwa muda wa nusu saa, ili kujenga afya na kujiepusha na magonjwa mbalimbali yakiwamo ya kisukari.

"Jamii ielewe kwamba mazoezi na kufanya kazi ni vitu viwili tofauti, kwa sababu wengine wakimaliza kufanya kazi wanasema wameshafanya mazoezi, waache dhana hiyo," alisema.

Watu wanaougua magonjwa yasioambukiza wamekuwa wakiongezeka siku hadi siku, huku serikali ikipigania kuondoa magonjwa hayo, ili kuwa na taifa lenye afya bora.

# Mtuhumiwa mauaji ya mchungaji wa KKKT kortini

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

HATIMAYE Naftari Lulandala, anayetuhumiwa kwa mauaji ya aliyekuwa mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Iringa, Elizabeth Ng'unga (36), amefikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Iringa.

Lulandala ambaye ni shemeji wa marehemu anatuhumiwa kufanya mauaji hayo Desemba 15, mwaka jana katika Kijiji cha Kipaduka, Wilaya ya Kilolo.

Shtaka hilo limekuja mbele ya Hakimu Mkuu Mkazi Mfawidhi wa Mkoa wa Iringa, Said Ally Mkasiwa na mshtakiwa hakutakiwa kukubali au kukataa kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Katika tukio hilo, baada ya Jeshi la Polisi kukuta mwili eneo la Kijiji cha Kipaduka walilazimika kupeleka mwili huo katika Hospitali ya Ilula Kilolo na baada ya kukaa muda mrefu bila ya ndugu kupatikana, serikali ya kijiji ililazimika kuomba hospitali hiyo kuuzika.

Hata hivyo, baada ya siku tatu, Aron Mkumbo, mume wa marehemu alijitokeza na kwenda Kituo cha Polisi cha Ilula kwa ajili ya kutoa taarifa ya kupotelewa na mke wake ndipo Jeshi la Polisi likalazimika kuufukua mwili huo na kumkabidhi mumewe kwenda kuuzika upya.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 17 ikisubiri upelelezi kukamilika na mtuhumiwa amerudishwa rumande kutokana na kosa hilo kutokuwa na dhamana.

Marehemu mchungaji Ng'unga, mzaliwa wa Ilambilole, alifanyia mazoezi huduma ya uchungaji Usharika wa Mlandege na kufanyakazi sharika za Luganga ya Ilula, Isimani - Kihorogota, Mfyome, Ndiuka, Mkwawa na ofisi kuu za KKKT Dayosisi ya Iringa kama Kasisi (Chaplain) Msaidizi hadi umauti ulipomfika.

Mchungaji Ng'unga aliuawa kikatili kwa kutobolewa macho eneo la Ilula, wilayani Kilolo.




Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, akisalimiana na baadhi ya wajumbe wa mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), uliofanyika kwa njia ya mtandao, katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: WAZARA YA MAMBO YA NDANI**

# Tunduru yapongezwa kukamilisha madarasa na kubakiza mil. 132/-

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKUU wa Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, amempongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Chiza Marando kwa kushirikiana na wataalamu wake kufanya kazi nzuri na kukamilisha kwa wakati ujenzi wa madarasa na kufanikiwa kubakiza Sh. 132,188,005.79 kati ya Sh. 2,916,514,747.00 zilizopokelewa na Serikali Kuu. Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 122 yakiwamo 113 ya shule za sekondari.

Akiwa anarejea maelekezo yaliyotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Mtatiro alimtaka Mkurugenzi huyo kukaa na wataalamu wake kupanga utaratibu mzuri wa kuzitumia fedha hizo kuimarisha miundombinu ya madarasa katika shule zenye uhitaji ndani ya wilaya yao.

Akitoa taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji Marando, alisema jumla ya Sh. 2,916,514,747.00 zilipokelewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 113 kwenye shule za sekondari 23 zilizoko wilayani humo zilizokuwa zimepangiwa Sh. 2,260,000,000.00.

Marando alifafanua kuwa kati ya fedha hizo ujenzi wa madarasa tisa kwenye shule za msingi shikizi tatu ambazo zilikuwa zimepangiwa Sh. 180,000,000.00 pamoja na ujenzi wa hosteli moja kwenye Shule ya Msingi Tunduru mchanganyiko yenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu iliyokuwa imepangiwa Sh. 80,000,000.00.

Pia alisema halmashauri yake ilipokea Sh. 396,514,747.00 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la huduma za dharura na nyumba ya mganga katika Kituo cha Afya Nalasi.

Alisema ujenzi huo ulianza Novemba 15, 2021 ulienda sambamba na utengenezaji wa seti 5,085 za viti na meza kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi umekamilika kwa asilimia 100 Desembe 27, mwaka jana na kwamba hadi kukamilika umegharimu Sh. 2,377,532,179.42.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Diwani wa Kata Mchangani, Haillu Mussa, alisema madarasa yote yaliyojengwa katika shule hizo yapo katika kiwango cha kisasa na ni ukombozi kwa wana Tunduru na kwamba mwaka huu hakuna mwanafunzi atakayebaki kutokana na kukosekana kwa madarasa. Alitoa wito kwa wazazi na walezi kuwasimamia watoto wao ili waende shuleni na wahakikishe wanamaliza masomo ili waje kuwasaidia baadaye.

Wakiongea kwa nyakati tofauti baadhi ya wakuu wa shule za sekondari, Niver Mbuza wa Shule ya Sekondari Mataka na Makrina Ngonyani wa Shule ya Sekondari Masonya, pamoja na ahadi ya kuyatunza madarasa hayo, walipongeza serikali kwa kuboresha miundombinu hiyo na kwamba kulingana na uwiano wa wanafunzi 40 hadi 50 kukaa kati ya darasa moja utafikiwa tofauti na awali darasa moja lilikuwa lina kaa wanafunzi hadi 100.

# Wawili wajitoa uhai kwa kujinyonga

**Na Neem Hussein,** KATAVI

WATU wawili wamekutwa wamefariki dunia kwa kujinyonga kwa nyakati tofauti mkoani Katavi.

Akithibitisha kutokea kwa matukio hayo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Hamad, aliwataja waliojinyonga kuwa ni Ndebi Samweli (35) na Edimondi Sungura (54), wakazi wa Manispaa ya Mpanda.

Alisema tukio la kujinyonga Ndebi lilitokea Desemba 31, 2021 katika kijiji cha Kasinde kwa kukutwa juu ya mti wa mwembe akiwa ametumia kamba aina ya manila.

Kamanda Hamad alisema chanzo cha kujinyonga ni wivu wa mapenzi baada ya kuacha ujumbe wa kumtuhumu mumewe, Jasula Masolwa, kumgombeza mara kwa mara pindi wake zake wengine wanapokosea.

Kamanda Hamad alitaja tukio lingine la kujinyonga la Edmond Sungura, kuwa lilifanyika chumbani kwake usiku wa kuamkia Januari 2, mwaka huu katika mtaa wa Rungwa, Kata ya Kazima.

Akizungumza na Nipashe mke wa marehemu, Astilida Makambila, alisema siku ya tukio mume wake aliamka asubuhi na kuelekea kwenye pombe na kurudi saa mbili usiku huku akiwafukuza yeye na watoto wake na kujifungia ndani ya chumba chake na kujinyonga.

"Aliporudi aliniita chumbani akaniambia tunza hizi simu, hii moja ni ya rafiki yangu atajiia kesho, nikatoka sebuleni nikaanza kuangalia TV, baadaye akatoka akasema naomba muondoke muende nje. Akazimisha Tv tukakaa nje, akaja tulipokaa akauliza hapa ndiyo nje au mnataka niwachafue? Basi nikatoka nikazunguka nyuma ya barabara, kidogo nikaona familia yote imenifuata. Nikauliza kulikoni, wakasema ametufukuza," alisema.

Aidha, alisema baada ya kurudi ndani majira ya saa sita usiku na kusukuma mlango wa chumbani, ulikuwa umefungwa wakajua amelala wakaingia chumba kingine na kulala, ilipofika asubuhi saa tatu na kuona hafungui mlango, aliamua kumuita huku akigonga mlango lakini hakuitika.

Alisema alichukua uamuzi wa kuvunja dirisha kwa panga na kuchungulia ndani na kumuona ananing'inia juu ya paa la nyumba.

Hata hivyo, alisema sio mara ya kwanza kwa marehemu kujaribu kufanya kitendo hicho na alikuwa akikizungumzia mara kwa mara kuwa ipo siku atakuja akifanye, wakati mwingine walijaribu hata kumwokoa wakati akijiandaa kufanya hivyo.

Kaka wa marehemu, Albin Sungura, anayeishi Mkoa wa Iringa, alisema mdogo wake alikuwa ana tabia ya kunywa pombe na kuwafokea, lakini yalikuwa yanaisha na kuendelea kuishi vizuri na familia.

Alisema tukio hilo ni la kwanza kutokea katika familia yao na katika mila na desturi zao wanaamini kuwa mtu akifariki kwa kujinyonga ni mkosi ndani ya nyumba na familia kwa ujumla.

"Mimi kama mkubwa wao ninalaani kitendo alichokifanya ndugu yangu kwani maisha aliyokuwa nayo si ya umaskini na sisi kama wanafamilia inabidi tufate mila. Hatustahili kulia, hairuhusiwi kumwombea, mwili hauagwi na familia, kuna dawa inatengenezwa kwa ajili ya zuio lolote baya la kuwazuru watu," alisema kaka wa marehemu.

Kwa upande wake mtoto wa marehemu, Filbert Sungura, alisema alipewa taarifa za kifo cha baba yake akiwa shambani na kabla ya kifo cha baba yake kulikuwa na ugomvi wa madai baina ya marehemu na mpangaji wake.

"Mzee wangu alikuwa anamdai mpangaji 50,000 ila huo ugomvi uliamriwa ukaisha walipelekana serikali za mitaa na akalipwa hela yake sasa baada ya hapo sikujua tena nini kiliendelea maana mimi sikai hapa," alisema.

Nipashe iliongea na Mwenyekiti wa Mtaa wa Rungwa, Mwelela Nkokwa, ambaye alisema alipigiwa simu na balozi wake akiwa anatokea kanisani kufika eneo la tukio baada ya kujiridhisha alipiga simu polisi kwa ajili ya taratibu zingine.

Alisema tukio hilo ni jaribio la tano kwa marehemu kutaka kujinyonga na amekuwa akipokea taarifa mara kwa mara kutoka kwa mke wake ambaye alikuwa akifika kwake na kumwambia mume wake anataka kujinyonga.

Alisema hilo ni tukio la pili kutokea katika mtaa huo na kutoa wito kwa wananchi wanapokuwa na changamoto washirikishe watu ili kubadilishana mawazo na kupeana moyo kusaidia kuepuka matukio kama hayo.



Mbunge wa Masasi ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Geoffrey Mwambe (aliyevaa kofia ya kijani), akitoa maelekezo kwa viongozi wa kata ya Temeke na watendaji wa Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara namna bora ya usimamizi wa ujenzi wa Sekondari ya Kata ya Temeke inayojengwa na serikali kwa zaidi ya Sh. milioni 100, jana. **PICHA HAMISI NASRI**

# Wanufaika TASAF washukuru kuinuliwa kimaisha

**Na Elizabeth Zaya**

WANUFAIKA wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), katika kijiji cha Kiparang`anda A, wilayani Mkuranga mkoani Pwani wameushukuru mfuko huo kwa kuchangia kuinua maisha yao.

Mariam Ali ambaye ni mmoja wa wanufaika wa mpango huo kutoka katika kijiji hicho, alisema tangu kupelekwa kwa mpango huo kijijini kwao kumekuwa na mabadiliko makubwa kwa maisha ya kaya za walengwa, tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema ruzuku wanayopatiwa imeowaongezea kipato na kuwa na uwezo wa kugharimia mahitaji muhimu ikiwamo kuwa na uhakika kupata milo mitatu ya chakula, kugharamia mahitaji ya shule kwa watoto wao pamoja na huduma za afya.

Pia alisema kupitia ruzuku hiyo, wamejifunza namna ya kujiwekea akiba na kuendesha shughuli ndogo za uzalishaji ikiwamo ufugaji wa kuku pamoja na kilimo.

Kwa upande wake, Mratibu wa TASAF Mkuranga, Safina Msemo, alisema kwa sasa kuna maendeleo mazuri ya wanafunzi kutoka katika kaya za walengwa kuhudhuria shuleni tofauti na kabla ya kuingizwa katika mpango.

"Na hata baadhi ya kaya wameunda vikundi vyao ambavyo vinashirikisha familia za walengwa pekee, ambavyo vinajishughulisha na kilimo cha muhogo na wamepata mafunzo ya kutengeneza bidhaa zinazotokana na zao hilo ikiwamo tambi, keki na unga na wanaziuza sehemu mbalimbali," alisema Msemo.

"Katika kijiji cha Kiparang`anda pekee, jumla ya vikundi vinne vya huduma ndogo za kifedha vimeundwa kupitia kaya za walengwa na vimeanza kufanya kazi ya kuweka akiba na kukopa fedha. Pia, vikundi vya walengwa vinavyolima muhogo katika vijiji vya Kiparang`anda A na B, Kizarapa, Lupondo, Mkelezange, njia nne Mikere na Misasa vimepata hamasa kwa kuwa na uhakika wa soko la unga wa muhogo kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkuranga."

Msemo alisema vikundi hivyo vimepewa mafunzo namna ya kuongeza mnyororo wa thamani katika zao hilo la muhogo na vimemudu kutengeneza bidhaa mbalimbali..

# Wavamizi wapigwa marufuku eneo la mitamba

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, amepiga marufuku ujenzi katika eneo la mitamba la serikali na kuonya wavamizi watakaokaidi agizo lake, watakuwa wamejipotezea muda wao.

Akizungumza na baadhi ya wananchi wanaodaiwa kuvamia eneo hilo, alikemea kitendo cha watu kuvamia maeneo ya serikali na yenye hatimiliki bila kufuata taratibu.

Alisema wapo watu wanatumia nguvu nyingi za kujenga kwenye maeneo yanayomilikiwa kihalali ambao baadaye wakivunjiwa wanarudishwa nyuma kimaendeleo.

"Hakuna hata siku moja serikali itakuja kuwaachia maeneo mlipovamia, hata kama itaacha itatoa kwenye mamlaka za upangaji yaani Mkurugenzi wa Halmashauri, hapo ni kwamba kama umejenga katika eneo la serikali ni sawa na mtu anayelala nje," alisema Sara.

Aliwataka wananchi kuheshimu ardhi za serikali na zinazotambulika kihalali na kuacha tabia ya kuvamia maeneo yasiyo ya haki kwao.

Aliwataka wavamizi kuondoka na kuacha kujenga eneo la Mitamba na kwamba atayekaidi na kuendelea atakuwa anajidanganya kuwa atapata haki ama kulipwa au kupewa eneo hilo.

ama
ALHAMISI JANUARI 6, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12


**KAMPENI YAPAMBA MOTO...**

Harakati zilivyotua kanisani, penye tiba asilia walikochanja na kujitolea ubalozi



Ukurasa 13

Waganga wa jadi wajitosa mapambano vifo wajawazito, watumiaji mitishamba



Ukurasa 14

**Ukosefu wa vyoo unavyokwamisha ubora wa uchimbaji migodi midogo**

# Namna ulivyo uhusiano wa maradhi akili na duru za uhusiano kimapenzi

• Milembe katika utafiti kufuatilia mzizi

**Na Yasmine Protace**

MATUKIO ya ukatili yanayoendelea kutoka kwa jamii, yanachangia kuwapo tatizo la afya ya akili duniani na sasa kumekuwapo baadhi ya watu wakipata changamoto za afya ya akili, hata ikagundulika kuwa zao la ukatili.

Mkurugenzi wa Tiba katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Omary Ubuguyu anasema kuongezeka tatizo afya ya akili kwa watu, kunasababishwa na matukio ya kikatili.

Pia, anasema baadhi ya magonjwa yanaweza yakaambatana na matukio ya kikatili kwa mhusika akiwa na ufafanuzi: "Kuna baadhi ya magonjwa ya akili yanaweza yakaambatana na tabia ya ukali."

Dk. Ubuguyu anasema kitendo cha mtu kuwa na hisia mbaya kwa mwenza wake kuhisi anamsaliti, ni hali inayomuweka pabaya kifikra, jambo linalorejesha haja kuwapo mawasiliano bora ndani na nje ya ndoa na jamii kwa upana.

Anaitafsiri familia ni taasisi pana, hivyo uimara wake unajengwa kwa ushirikiano kati ya wenza, huku ubora wao unaimarishwa kwa mawasiliano ndani na nje ya matatizo ya wenza, hivyo ni lazima yajadiliwe kuepusha afya ya akili kwa familia na kudhibiti matatizo aina hiyo.

"Mtu asiyekua na afya njema ya akili, anaweza akawa mgonjwa wa akili au anaweza kushindwa tu kudhibiti hisia zake na hawezi kupima fikra zake kwa kujua jambo linaweza kuwa na madhara kiasi gani," anafafanua Dk. Ubuguyu

Pia, anawataka wazazi na walezi wasikasirike kila mara mbele ya watoto, kwani sehemu ya malezi inachangia kuumiza hisia za watoto, hata kuchangia wakajifunza wakihisi ndio njia sahihi za kukabiliana na kero hizo.

"Jamii bado inashindwa kuripoti watu wenye matatizo kwa kuhofu au kumuogopa mtu mwenye dalili, ili kudhibiti watu wenye matatizo ya afya ya akili kwenye jamii, lakini atakapofanya tukio la kikatili, basi jamii inayomzunguka itasema walihisi na kuona dalili," anasema.

Dk. Ubuguyu anabainisha kuwa serikali kupitia Wizara ya Afya, imetoa kipaumbele kwa kuweka waratibu kitaifa na mkoa, penye halmashauri na maeneo ya kutoa huduma za afya, kuanzia Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Kimsingi, huduma za afya ya akili zinatolewa hapo na wananchi wasisite kufika kwenye vituo vya afya kupatiwa huduma ili kuepuka matukio ya kikatili kwenye jamii.



Daktari bingwa wa magonjwa ya akili, kutoka Hospitali ya Afya ya Akili Milembe Dodoma, Inocent Mwombeki. **PICHA: YASMINE PROTACE**

**ZILIVYO DALILI ZAKE**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Akili katika Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Innocent Mwombeki, anafafanua kuwa dalili za ugonjwa wa afya ya akili, ni pamoja na kubadilika tabia, hasira za karibu na kusikia sauti za watu kuongelesha pasipo kuwaona.

"Dalili zote hizi hupelekea mtu kupatwa na ugonjwa wa afya ya akili, pia ugonjwa huo unatibika kwa kupata dawa pamoja na kusikiliza wataalamu wa saikolojia," anasema.

Dk. Mwombeki anafafanua kuhusu matibabu ya dawa hiyo, kwamba mtu anaweza kupona ndani ya muda mfupi na kurudi katika hali ya kawaida, japo wengine huchukua muda kutokana na aina ya ugonjwa alio nao.

"Tumeanzisha kitengo kipya cha utafiti na mafunzo kwenda kwa jamii na tayari tafiti zilishafanyika kwa watu zaidi ya 180 kwenye mikoa tafauti.

"Asilimia 32 tuliwakuta na dalili za magonjwa ya akili na asilimia 10 walikua na matumizi mabaya ya pombe na asilimia 19 walishawahi kupata wazo la kutaka kujiua," anaeleza Dk. Mwombeki

Anafafanua kwamba wagonjwa wote wanatakiwa kutibiwa ndani ya maeneo yao kama ni mkoani, wilayani na mgonjwa akilazimika kutoka ndani ya mkoa husika, basi anatakiwa kuwa na mtu wa karibu kwa ajili ya uangalizi.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), inakadiriwa katika kila sekunde 40 mtu mmoja anafanya tukio la kukatisha uhai wake, huku wengine 800,000 wanakatisha maisha duniani kila mwaka.

AFYA

KAMPENI YAPAMBA MOTO...

# Harakati zilivyotua kanisani, penye tiba asilia walikochanja na kujitolea ubalozi

• Singida, kutoka 'kuharibu' hadi mfano kitaifa

**Na Mary Geofrey, aliyekuwa Singida**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imefunga mwaka kwa kuzindua Kampeni ya Uhamasishaji na Utoaji wa Chanjo ya Uviko -19, katika Mpango Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili.

Mpango huo unaotekelezwa na wizara kupitia Kitengo cha Elimu kwa Umma, Desemba 22 mwaka huu, ilizindua Kampeni ya Uhamasishaji na Utoaji Chanjo ya Uviko VIKO-19, awamu ya pili ya mpango huo unaotekelezwa na wizara hiyo, Kitengo cha Elimu kwa Umma.

Waziri Dk. Dorothy Gwajima, amezindua kampeni katika kiwanja cha Ngarenaro mkoani Arusha, iliyotanguliwa na mafunzo kwa maofisa afya kuhusu utekelezaji kampeni hiyo. Ni aina ya malengo yanayohusisha viongozi wa dini, serikali mitaa, vitongoji, vijiji na mila kwa ujumla wanaohusika na wananchi moja kwa moja.

Waziri Dk. Gwajima, anasema kampeni inalenga kuwachanja watu majumbani, shambani, kazini, magulioni, ibadani na kote waliko wananchi.

## HARAKATI ZA SINGIDA

Singida, Manyara, Njombe, Iringa na Ruvuma inatajwa kuwa mikoa mitano iliyofanya vibaya katika awamu ya kwanza ya mpango shirikishi na harakishi wa chanjo.

Kampeni iliyofanyika kwa siku saba mkoani Singida, iliendeshwa na wataalamu wa afya kutoka wizarani kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), pia ngazi ya mkoa, hata wakawafikia matabibu asilia na waumini wa madhehebu.

Wakati wa Sikukuu ya Krismasi zaidi ya wiki moja na nusu iliyopita, Nipashe ilishuhudia wataalamu wa afya waliojitokeza kuwafuata waumini ibadani kuwapatia chanjo iliyopo sasa, aina ya Pfizer.

Baada tu ya kumalizika ibada katika Kanisa ya Kiinjili ya Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Imani, pia Kanisa Katoliki Parokia ya Yohana Mbatizaji Mtinko na Kanisa la Pentekoste FPCT Ilongero, wilayani Singida mkoani Singida, waumini walijitokeza kupata chanjo hizo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Victorina Lodovick, kwa nyakati tofauti makanisani, anawahimiza waumini kusherehekea Krismasi, kuendana na kupata chanjo ya Uviko -19.

Dk. Victorina anasema, ni wajibu wa serikali kuhakikisha usalama wa raia wake, hivyo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inaendeleza kampeni za 'nyumba kwa nyumba' pia ' mtaa kwa mtaa' kuwafikia wananchi wahitaji wa chanjo, mkoa wote wa Singida.



Namna kampeni ya chanjo za papo kwa hapo mkoani Singida, ikijumuisha nyumba za ibada na waliko matabibu asilia. **PICHA: MARY GEOFREY**

> **Nasi tumeamua kuwa mabalozi kwa wateja wetu, lakini pia na waganga wenzetu, ambao hawajapata chanjo ili tuendelee kutoa huduma tukiwa salama na wateja wetu nao wawe salama.**

Paroko Msaidizi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Yohane Mbatizaji Mtinko, Padri Raphael Madinda, anasema walishapatiwa mafunzo kuhusu tahadhari ya ugonjwa huo na chanjo ya Uviko -19 kutoka Wizara ya Afya na ndio sababu nao wanaendeleza elimu kwa waumini wao.

Rai yake anawataka waumini wasipuuze taarifa zinazotolewa na wataalamu wa afya, hasa kwa kuzingatia ilikuwa 'Sikukuu ya Familia Takatifu ya Mungu' yaani Mariam, Yoseph na Yesu waliokuwa mfano wa kuigwa.

"Kama ilivyo mfano kwa Familia Takatifu ya Mungu, nanyi tunawasihi wanafamilia kuzilinda familia zenu kwa kujikinga na maradhi haya, lakini pia kupata chanjo ya Uviko -19," anahimiza Padri Madinda.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mtakatifu Carolus Mtinko, Sister Dk. Susanna Mushi, anatumia fursa hiyo, kuwahimiza waumini kuwa mgonjwa Uviko -19 aliyezidiwa anatakiwa kuwekewa mitungi ya gesi, ambayo haipatikani kirahisi wilayani humo.

Anasema kila mgonjwa anatumia wastani wa mtungi mmoja kwa saa nane na gharama zake ni kubwa ambazo wananchi wengi hawazimudu.

"Kwanini tufike huko? Tujitokeze kuchanja, ili kuwa na uhakika wa usalama wa maisha yetu. Ukichanja huwezi kuzidiwa na utaisadia familia yako inayokutegemea," anasema Sister Dk. Susanna.

## AWAMU YA KUCHANJA

Askofu wa Kanisa la Pentekoste FPCT, Wilson Lazaro, anawaongoza waumini wake kupata chanjo ya Uviko -19, akianika msimamo wa kanisa 'ni kuchanja' na 'kuondokana na dhana potofu kuhusu chanjo zinazotolewa.'

Waumini wa KKKT Usharika wa Amani wakapata fursa ya kuuliza maswali mbalimbali, ikiwamo "kama wanaweza kunywa pombe baada ya kuchoma chanjo?" vivyo hivyo, "wajawazito nao wananyonyesha? kama wanaruhusiwa na wenye maradhi sugu chanjo hiyo haitawasumbua?..."

Baada ya kupatiwa majibu safi na wataalamu wa afya kutoka serikalini, walianza kuchanja mara moja. Hapo, Maria Emmanuel, muumini wa KKKT Usharika wa Amani, anaishukuru serikali kuwafumbua macho wao waumini kuhusu mustakabali wa Uviko - 19.

"Mmetuelimisha na kujiridhisha kuwa chanjo ni salama, tunaamini mtaendelea kuelimisha na waumini wa madhehebu mengine ili nao wachanje," anasema Maria.

## WAGANGA WA JADI

Kampeni ilitua hadi penye ulingo wa tiba asilia, pale waganga wa jadi 28 katika kata ya Ipande, halmashauri ya Itigi, wilayani Manyoni walikubali kuchanja dhidi ya Uviko -19, sambamba na kujitolea kuwa mabalozi wa chanjo hiyo inayoendelea nchini kote.

Nao wakaeleza msimamo waliojijengea kwamba, hawatokuwa tayari kutoa tiba kwa wagonjwa ambao hawajachanjwa. Nyanza Ndambuli, Katibu wa Waganga wa Tiba Asili katika kata ya Ipande, anasema wameamua kuchanja na kutoa elimu kwa wateja wao, baada ya kuelimika kuhusu chanjo UVIKO-19, wakiahidi kuwa mabalozi bora wa kampeni ya chanjo waliko.

"Kwa pamoja kama waganga wa tiba asili tumekubaliana kutoa elimu kwa wateja wetu pia. Kwa siku napokea wateja kuanzia wanne, ina maana akija mteja mwenye corona ni rahisi kuniambukiza na kuambukiza wengine, lakini tukichanja tunakuwa salama wote," anasema Ndambuli.

Mtafiti wa Tiba Asili kata ya Ipande, Hussen Rajabu, anasema walipatiwa elimu ya chanjo na walikubali kuchanja, hivyo wapo tayari kuwahamasisha waganga wengine wapate chanjo hiyo.

"Tulikutana na waganga 28 na wote kwa umoja wetu tulikubali kupata chanjo ya UVIKO-19. Tumekubaliana kuanza kuzungumza na wateja wetu kwanza wakapate chanjo ndio tuwapatie matibabu ili kuepuka kuenea kwa ugonjwa huu," anasema.

Katibu wa Waganga wa Tiba Asili, Halmashauri ya Itigi, Halima Mbalamwezi, anaishukuru serikali kwa kutambua umuhimu wa waganga wa kienyeji na kuamua kuwapatia elimu ya chanjo na kuwachanja.

"Nasi tumeamua kuwa mabalozi kwa wateja wetu, lakini pia na waganga wenzetu, ambao hawajapata chanjo ili tuendelee kutoa huduma tukiwa salama na wateja wetu nao wawe salama," anasema.

Diwani wa kata ya Ipande, Kedmon Mpondo, anasema kwa kushirikiana na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Itingi, Emmanuel Mallange, walifanya kikao na waganga hao wa tiba asili kuwapa elimu ya chanjo ya UVIKO-19.

Mwenyekiti wa Huduma za Afya katika halmashauri hiyo, anaahidi kuendelea na kazi ya kuwafikia waganga wengine waliobaki katika kata yake.

"Tunaamini kuwa kuwafikia waganga hawa, nao watawafikishia taarifa wenzao na wateja wanaoenda kuwapatia matibabu katika maeneo yao," anasema Mpondo.

Kampeni hiyo inalenga kufikia wananchi nyumbani, mtaani, shambani na sehemu za biashara, inatekelezwa na wizara hiyo kupitia Kitengo cha Elimu kwa Umma na lengo ni kufikia asilimia 60 ya Watanzania.

AFYA

# Waganga wa jadi wajitosa mapambano vifo wajawazito, watumiaji mitishamba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

- Mteja wao akifika anaelekezwa zahanati
- Wajiwekea sheria, anayekiuka adhabu

MATUMIZI ya dawa za miti shamba kwa wajawazito katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, limekuwa tatizo kubwa linalokosa ufumbuzi wa haraka, hata kusababisha kuendelea kuwapo vifo vya wajawazito na watoto wachanga kila mwaka.

Dawa hizo zimekuwa zikitumiwa vibaya na wajawazito, hali inayoletea shida ya kiafya, hasa katika kutibu shida kama za minyoo na kuongeza uchungu. Pia, kitaalamu inafafanuliwa imekuwa ikisababisha mfuko wa uzazi kupasuka na mtoto kunywa maji machafu tumboni.

Inatajwa sehemu kubwa ya wajawazito hao watumiaji wa mitishamba ni wanaotoka pembezoni mwa miji, wakipata shinikizo la maelekezo ya wazazi wao, kwamba huko nyuma nao walizitumia kwa mafanikio.

Hata hivyo, inatajwa huko nyuma dawa hizo zilitumika zaidi kutokana na uhaba wa vituo vya afya nchini, lakini kwa sasa huduma hizo zimesambaa sehemu nyingi kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ambao una miaka 13 tangu uanze kutekelezwa.

Kwa mujibu wa MMAM, kila kijiji au kitongoji kinapaswa kuwa na zahanati, hali kadhalika kituo cha afya kwa kata, wilaya inakuwa na hospitali, mkoa hospitali ya rufani, vivyo hivyo hospitali za rufani za kanda na juu kuna Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).



Kinamama wenye watoto chini ya miaka mitano wakisubiri kuonana na daktari kwa ajili ya ukaguzi wa maendeleo ya afya ya watoto wao, Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

**TIBA ASILI WAIBUKA**

Hadi sasa, Shirikisho la Tiba Asili Kanda ya Magharibi, inayojumuisha mikoa ya Kigoma, Shinyanga na Tabora, imeamua kujitosa kupambana na matumizi ya dawa za asili kwa wajawazito, ili kuondokana na vifo hivyo vilivyokuwa vikijitokeza, pale wajawazito wanapotumia dawa za kuongeza uchungu.

Shirikisho hilo limekuwa likitoa maelekezo kwa wakunga wa tiba asili, katika namna ya utoaji huduma kwa wananchi na wateja wajawazito hawatakiwi kupewa dawa za namna hiyo, badala yake wanawashauri kwenda kituo cha kutoa huduma kwa matibabu zaidi.

Athumani Waziri, Mratibu wa Shirikisho la Tiba Asili Kanda ya Magharibi, anajitambulisha kuwa wao ni miongoni mwa wanaopinga matumizi ya dawa hizo kwa wajawazito, kwani kila inapotokea tatizo kwa wajawazito na watoto wachanga, wamekuwa wakipokea lawama wao.

Anasema dawa hizo ni kali sana, hata mjamzito anapozitumia kuongeza uchungu, kuna wakati zinachangia mfuko wa uzazi uliombeba mtoto kuchanika na mtoto tumboni kunywa maji machafu, hata kumpotezea maisha, huku kukiwapo mikasa mzazi na mtoto kupoteza maisha pamoja.

> **Wajawazito waliojifungua mwaka jana katika hospitali ya halmashauri hiyo mwaka jana walikuwa 16,008. Katika orodha yao, anawataja 115 walizaliwa na mwili ulioharibika.**

Waziri anaendelea kueleza kuwa wajawazito wanaoishi vijijini wanapopata matatizo ya uzazi, mara nyingi wanakimbilia kwa waganga wa jadi, badala ya vituo vya afya vilivyopo jirani, hali inayosababisha kupewa dawa za mitishamba inayoishia penye madhara.

Anasisitiza katika vikao vyao vya kila siku, wanakumbushana wajibu wa kazi zao, namna ya kupambana na vifo hivyo kwa kuwataka wakunga wao wanapopata wateja wajawazito, wanawaelekeza katika vituo vya afya kupata ushauri zaidi.

Lililo chanya katika ufafanuzi wake ni kwamba: "Mpaka sasa hatujapata kesi yoyote ya mkunga wetu kumpatia mjamzito dawa za kutibu minyoo au kuongeza uchungu. Tuna kamati yetu ya maadili ambayo mkunga akifanya tofauti na maadili yetu, tunamchukulia hatua za kinidhamu."

**MRATIBU MAMA/MTOTO**

Caroline Maliseli, ni Mratibu wa Afya ya Mama na Mtoto Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, anasema katika wodi za kinamama wamekuwa wakiwakamata wajawazito wanaofika hospitalini kujifungua wakiwa na dawa za kuongeza uchungu zilizosagwa na wanazitumia kwa kuchanganya na chai.



Mratibu wa Afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Caroline Maliseli.

Anasema wanapowahoji baada ya kuwanasa, wanajitetea zinawaongezea uchungu wanajifungua haraka na wanapatiwa na wazazi wao wanaowasisitizia uzoefu wao ziliwafaa katika uzazi wao.

Mratibu huyo anatoa takwimu, kwamba mwaka jana watoto wachanga 436 na wajawazito sita walipoteza maisha katika eneo lao, sababu mojawapo ni matumizi ya dawa za mitishamba na ndio maana wanawashirikisha matabibu asilia, katika vita hivyo.

**VIFO VYA VICHANGA**

Caroline anafafanua kwamba, mwaka jana watoto 31 walizaliwa wakiwa na ulemavu wa vichwa vikubwa, mgongo wazi, tumbo wazi, matege na matatizo mengine kutokana na mama zao, kuhudhuria kliniki wakiwa wamechelewa kwa zaidi ya miezi mitatu na kushindwa kutumia dawa wanazopatiwa kipindi cha ujauzito.

Anasema, wajawazito waliojifungua mwaka jana katika hospitali ya halmashauri hiyo mwaka jana walikuwa 16,008. Katika orodha yao, anawataja 115 walizaliwa na mwili ulioharibika.

Pia, anataja idadi ya waliozaliwa na kufa ndani ya siku saba walikuwa 58. huku vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi vikiwa tisa.

Anafafanua vifo vya watoto chini ya mwezi mmoja vilikuwa sita, chini ya mwaka mmoja vifo 29 na chini ya miaka mitano vikiwa vifo 105.

Mwaka juzi vilikuwapo vifo vya watoto na kinamama 456 sawa na ongezeko la vifo 10 mwaka huu.

Vilevile, anasema kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba mwaka jana, kuna watoto wachanga 31 waliozaliwa na ulemavu wa vichwa vikubwa, mgongo wazi, tumbo wazi na matatizo mengine, chanzo kikubwa kikitajwa ni wazazi wao kuhudhuria kliniki baada ya miezi mitatu wakishindwa kupata dawa zinazotakiwa kutumiwa kipindi cha ujauzito.

Katika hilo, Caroline anataja sababu za kuwapo vifo vingi, ni wajawazito kutokuhudhuria kliniki kwa wakati na wanatumia dawa za asili, licha ya kuendelea kupewa elimu ya athari zake kila wanapohudhuria kliniki.

Karibuni alileta mjamzito akiwa katika hali mbaya akiwa ametumia dawa za mitishamba kwa kuongeza uchungu wa kujifungua. Tulimsaidia na tukamuokoa yeye, mtoto tayari alikuwa ameshapoteza maisha tumboni," anafafanua Caroline.

Anaeleza kwamba ili kuondokana na tatizo hilo, mjamzito anatakiwa kuhudhuria kliniki anapopata dalili za ujauzito na kuhakikisha anahudhuria kipindi chote cha ujauzito na muda utakapofika wa kujifungua, ahakikishe anahudhuria katika kituo cha afya.

Mama huyo mtaalamu anaitaka serikali ya mtaa kwa kushirikiana na watendaji wake, wajiwekee sheria kuwabana wajawazito wasiohudhuria kliniki kipindi cha ujauzito, wakiwamo wanaokimbilia kwa waganga wa jadi, waangukie adhabu za faini kisheria, ili kuleta nafuu ya madhara hayo.

Pia, anashauri sheria hiyo, iwabane wazazi na walezi wanaowarubuni wajawazito kutumia mitishamba kuongeza uchungu au kutibu minyoo kipindi cha ujauzito.

MAZINGIRA

# Ukosefu wa vyoo unavyokwamisha ubora wa uchimbaji migodi midogo

• Penye hitaji, wanamalizia vichakani; wamlilia waziri, awajibu 'kazi ya DED'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa madini na hasa dhahabu wamedumu kuwa nguzo muhimu ya uchumi wa nchi, wako katika wasifu kuwa chanzo cha huduma jirani waliko na eneo lao la kazi elimu, afya, maji na miundombinu ya barabara.

Ni kundi linalochangia pato la taifa kwa asilimia 7.1 na linatoa ajira za moja kwa moja kwa Watanzania wanaokadiriwa 680,000, ikilinganishwa na 8,800 walioajiriwa na wachimbaji wakubwa.

Pia, inakadiriwa kila mchimbaji mdogo anazalisha ajira ya wengine wanne, hivyo kulifanya eneo hilo la uchumi wa taifa kuajiri Watanzania wapatao milioni tatu, wengi wanaishi vijijini.

Hata hivyo, kazi zao zinalalamikiwa kuathiri mazingira kwa kutiririsha maji yanayosadikika kuwa na sumu ya kukamata dhahabu kwenye makazi yanayowazunguka, wachimbaji wakishindwa kufuata viwango vya afya na usalama mahali pa kazi.

Hadi sasa mkoa wa kimadini wa Kahama, una jumla ya leseni za uchimbaji mdogo wa madini 592, Halmashauri zake, Ushetu ikiwa na leseni 111, Manispaa Kahama 48 na Msalala 433.

Katika mgawanyiko huo leseni 568 ni za uchimbaji dhahabu na 12 za madini ya ujenzi, huku leseni zingine 12 ni kwa ajili ya kuchimba almasi.

### KILIO CHA VYOO

Katika mustakabali wa afya na mazingira, hapo ndipo penye shida. Katika mgodi mdogo wa Ntambalale kijijini Wisolele, ndani ya Halmashauri ya Msalala kuna migodi yenye leseni, lakini unabakiwa na changamoto ya ukosefu wa huduma za choo.

Ni hali inayowafanya wachimbaji wake waendelee kujisaidia vichakani, hata kutishia kuwapo magonjwa ya milipuko.

Kukosekana huduma ya vyoo, kumewafanya wachimbaji wadogo mgodini kuangua vilio mbele ya Waziri wa Madini Dk. Doto Biteko, wakimuomba awasaidie kupata huduma ya vyoo wakijisaidia vichakani, jambo lililo hatari kwa afya zao.

Nestory Masale, mchimbaji mdogo wa mgodi wa Ntambalale, anasema kwa sasa hawana huduma ya choo kwa ajili ya wachimbaji na wageni wanaowatembelea, badala yake wanajisaidia vichakani, hali inayotishia kuwapo ugonjwa wa kipindupindu



Waziri wa Madini Dk. Doto Biteko, akizungumza na wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Mgodi wa Ntambalale, Halmashauri ya Msalala, Shinyanga. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

> **Sehemu ya migodi ya halmashauri inachukua mapato kwa mujibu wa sheria ndogo walizojiwekea, hivyo mkurugenzi anatakiwa kutatua changamoto zinazopatikana katika maeneo hayo.**



Wachimbaji madini wadogo katika mgodi wa Ntambalale kijijini Wisolele, Halmashauri ya Msalala, Shinyanga wakisukuma rola kuvuta mifuko ya mawe yanayosadikiwa kuwa na madini.

kwa kipindi cha mvua za masika.

Masale anatahadharisha hatari iliyoko kutokana na kujisaidia vichakani wakati wa mvua, kunazua uwezekano vinyesi na haja ndogo kutiririka kwenye vyanzo vya maji, hata kuziathiri jamii zinazowanguka na kutumia maji yasiyo salama inaishia kusababisha magonjwa hatari.

Mchimbaji huyo anaendelea kufafanua kuwa, licha ya wao kuzalisha kwa wingi na kuiingizia Halmashauri ya Msalala mapato makubwa bado halmashauri hiyo inashindwa kuwajengea vyoo vya kuwasitiri wachimbaji na wageni wanaowatembelea kuwa na afya njema na kuongeza uzalishaji zaidi.

Stephen Kasiga, anasema uchimbaji madini unatakiwa kwenda sambamba na afya njema, hivyo kukosekana huduma ya choo ni kukaribisha magonjwa ya mlipuko kwa wachimbaji, hata wanashindwa kuzalisha na serikali inakosa mapato.

Anashauri serikali kuitazama hali hiyo na kuitafutia ufumbuzi haraka, ili kulinda afya za wachimbaji wanaoipatia serikali mapato, kwani anaielezea ni fedheha, kwa sasa mgodi hauna choo na serikali inaendelea kukusanya mapato na kushindwa kujali afya zao.

Waziri wa Madini Dk. Doto Biteko, analizungumzia hilo kwamba ni jambo ambalo ngazi ya utatuzi wake iko katika mamlaka ya wakurugenzi wa halmashauri husika, kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Kahama.

Anasema, sehemu ya migodi halmashauri inachukua mapato kwa mujibu wa sheria ndogo walizojiwekea, hivyo mkurugenzi anatakiwa kutatua changamoto zinazopatikana katika maeneo hayo, ikiwamo ujenzi wa vyoo na barabara, ili aendelee kukusanya kodi bila malalamiko ya wachimbaji.

Dk. Biteko anawapongeza viongozi wa mgodi kujenga zahanati ya kijiji inayotumika kuwahudumia wachimbaji wenye matatizo kazini, ikiwajumuisha wanaozunguka mgodi huo.

### DC NA DED KAHAMA

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, baada ya kilio hicho, anatoa siku 14 kwa wenyeviti wa wachimbaji wadogo na wamiliki leseni, kuhakikisha wanajenga vyoo haraka na baada ya muda huo, ataanza kukagua migodi kuangalia uwapo wa huduma.

Anatahadharisha, pindi anakuta mgodi usio na huduma ya choo kwa muda alioutoa, atachukua hatua ya kuwawajibisha kisheria viongozi wa migodi, kwa sababu unaaminika kuwa ukiukwaji wa masharti ya leseni zao, yanayotaka penye uchimbaji mdogo pawepo choo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Msalala, Charlse Fussi, anaahidi kushirikiana na viongozi wa migodi hiyo, kuhakikisha wanatengeneza barabara zinazounganisha migodi, ili kurahisisha usafirishaji mawe yanayosadikiwa kuwa na madini.

### UJENZI ZA WA ZAHANATI

Mwenyekiti wa Mgodi, Hamisi Mabubu anasema wamejenga zahanati katika kijiji cha Wisolele, jirani na mgodi kwa thamani ya shilingi milioni 45, inayowahudumia wananchi wanaopatwa na matatizo kwa huduma ya kwanza, kabla ya kupelekwa hospitali ya wilaya kwa matibabu zaidi.

Anasema, awali kabla ya ujenzi wa zahanati hiyo, wananchi walitembea umbali kilometa 14 kwenda zahanati ya kata ya Segese kupata huduma na kuna wakati wajawazito walishindwa kuhudhuria kliniki kipindi cha ujauzito na kujifungua majumbani, jambo ambalo ni hatari.

Hamisi anafafanua kwamba wanaendelea kupata huduma ya kwanza zahanati hapo wanapoumia, na kwamba wametenga gari maalumu la kuwasogeza katika kituo cha afya wachimbaji wanaotakiwa kupata huduma zaidi hospitali ya wilaya.



## Mradi wachangia kina mama kwenda kuhudhuria kliniki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MRADI wa Mama na Mtoto unaofadhiliwa na shirika lisilo la kiserikali la World Vision unaotekelezwa mkoani Dodoma, umechangia kwa kiasi kikubwa kutoa msukumo kwa kinamama vijijini kuhudhuria kliniki kwa ajili ya kuangalia afya ya mtoto.

Kabla ya mradi huo kinamama wengi vijijini walikuwa hawaendi kliniki na badala yake kujifungulia nyumbani jambo ambalo lilihatarisha maisha yao na kiumbe kinachozaliwa.

Kutokana na hali hiyo, World Vision iliamua kuanzisha mradi huo ikiwamo kutoa vifaa vya msaada vya hospitali ili kuwavutia kinamama kuhudhuria kliniki jambo ambalo walifanikiwa kwa asilimia 100 kutokana na mahudhurio yaliyopatikana.

Meneja wa Mradi wa Mama na Mtoto kutoka shirika hilo, Daudi Gambo, alisema hivi sasa imekuwa kama desturi katika vijiji mbalimbali mkoani Dodoma kuona kinamama wakihudhuria kliniki na watoto wao kwa ajili ya kuangalia afya za watoto pamoja na kupima uzito ili kupata ushauri nasaha wa lishe bora itakayomsaidia mtoto kukua vizuri kiafya.

Alisema wilaya ambazo mradi huo unatekelezwa mkoani hapa ni Bahi, Chemba na Kondoa.

Alisema suala hilo ni moja ya mkakati kabambe wa World Vision ambao wamefanikiwa kuokoa vifo vya mama wajawazito na watoto wanaozaliwa kutokana na kuwaweka katika mazingira mazuri hivi sasa tofauti na mwanzo.

Gambo alisema World Vision iliamua kuanzisha mradi huo baada ya kuona watoto wengi wanakumbana na utapiamlo kwa sababu wazazi wao hawajui kutengeneza lishe bora ndio maana wakaona wabuni mradi huo ili kuwasaidia wajawazito na wale ambao tayari wameshajifungua.

Alisema baada ya kuanzisha mradi huo waliwafundisha baadhi ya wahudumu ngazi ya vijiji ili waweze kuwasaidia wenzao katika kuhakikisha wanatoa mafunzo kwa kinamama hao ili kuhudhuria kliniki na kupata elimu ya utunzaji mtoto.

# Kampuni zisizowasilisha taarifa kikaangoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema itazichukulia hatua za kisheria kampuni zitakazoshindwa kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa ndani ya muda uliopangwa.

Pia imesema inatarajia kutoa taarifa ya sensa ya kampuni zilizopo nchini ifikapo Februari, mwaka huu.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu kuongeza muda wa miezi sita kwa ajili ya kuwasilishwa taarifa hizo.

Alisema awali taarifa hizo zilipaswa kuwa zimewasilishwa ifikapo Desemba 31, mwaka jana lakini kutokana na maombi ya wawekezaji kuhusu kuongeza muda, serikali imeongeza miezi sita ili kutoa nafasi kwa wamiliki hao kuwasilisha taarifa zao.

Prof. Mkumbo alisema kampuni zilizowasilisha taarifa hadi jana ni 14,026 sawa na asilimia 14 ya matarajio. Alisema kampuni zote nchini husajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na hupaswa kutoa taarifa kadhaa ikiwamo wamiliki manufaa wa kampuni.

"Awali ilikuwa hulazimiki kisheria kutoa taarifa za walioko nyuma ya kampuni yaani wamiliki manufaa na hawa ndio wenye mtaji na wanaendesha kampuni, hivyo Benki ya Dunia na taasisi zingine kimataifa zimehimiza kueleza kwa uwazi umiliki wa kampuni," alisema.

Alisema kutokana na umuhimu wa taarifa hizo na kwa mamlaka aliyo nayo kisheria, ameongeza muda hadi Juni 30, mwaka huu, ili wamiliki wote watimize matakwa ya kisheria.

"Niwahimize wamiliki wote watumie muda vizuri wa nyongeza na sheria iko wazi kwa yule ambaye hatawasilisha taarifa zake hatua gani zitachukuliwa dhidi yake. Katika kujenga uhusiano mwema na wafanyabiashara, tumekubaliana kuongeza muda huu," alisema na kusisitiza kuwa baada ya muda huo kwisha, sheria itatekelezwa kikamilifu.

Kuhusu sensa, Prof. Mkumbo alisema inafanywa na BRELA kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na ilianza Desemba mwaka jana na ifikapo Februari mwaka huu takwimu zitatolewa na kampuni.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kampuni na Majina ya Biashara kutoka BRELA, Meinrad Rweyemamu, alisema sheria ya kampuni imeweka utaratibu pale ambapo mtu atachelewesha kuwasilisha taarifa atakumbana na adhabu ya kulipa Sh.2,500 kila mwezi.

"Kwa kila mwezi ambao atakuwa amechelewesha taarifa atapaswa kulipa kiasi hicho, sambamba na hilo ikibainika haikuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa au kuwasilisha taarifa ambazo si za kweli mahakama itaipiga adhabu kampuni hiyo ya faini kuanzia Sh. milioni tano hadi 10,"alisema.

Alisema kampuni ambazo zimekuwa zikipeleka taarifa za mwaka ni zaidi ya 140,000 na kwamba bado nyingi hazipeleki taarifa, hivyo wanatarajia kutoa taarifa ya kampuni zisizo hai ili zihuishe taarifa zao.




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Dk. Ashatu Kijaji ambaye ni Mbunge wa Kondoa Vijijini, akipanda mti kuashiria uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti katika Jimbo la Kondoa Vijijini. **PICHA PAUL MABEJA**

# Dk. Kijaji aanza mwaka 2022 na upandaji miti

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, amezindua kampeni ya upandaji miti kwenye jimbo la Kondoa ikiwa ni mkakati wa kitaifa kuifanya nchi kuwa ya kijani.

Tukio hilo la uzinduzi lilifanyika juzi katika kata ya Hondomairo kwenye shule ya sekondari Hondomairo na shule ya msingi shikizi ya Misrey.

Katika tukio hilo, Dk. Ashatu alifuatana na viongozi mbalimbali wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Dk. Hamisi Mkanachi.

Katika uzinduzi huo, Dk. Kijaji aliongoza kwa kupanda zaidi ya miche 2,500 kuzunguka shule hizo.

Akizungumza na wananchi wa maeneo hayo baada ya kupanda miti hiyo, Dk. Kijaji alisema suala la utunzaji wa mazingira ni jukumu la kila mwananchi, hivyo agenda ya upandaji miti iwe endelevu.

"Tunatamani kuiona Kondoa yetu ya kijani ndiyo maana tumesema hili tulianze siku ya kwanza ya mwaka 2022 tuanzie hapa Misrey ili tuendelee kwa pamoja kuifanya Misrey ya kijani, Kondoa ya kijani na taifa letu la kijani. Mazingira yetu ni muhimu sana, miti yetu ni muhimu sana ndiyo maana tunaona leo (juzi) tunapata mvua za kusuasua sababu ya kuharibu mazingira yetu," alisema Dk. Kijaji.

Pia alisema anatamani kuona Kondoa ya kijani na Dodoma ya kijani na hatimaye nchi kuwa ya kijani kwa kila mmoja kuwajibika kupanda miti katika eneo lake na kuitunza hali ambayo itasaidia kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Katika hatua nyingine, alisisitiza suala la wazazi kuwapeleka watoto shuleni kwa kuwa hakuna tena kikwazo kwa kuwa miundombinu ya shule hiyo shikizi imekamilika vizuri na vyumba vya madarasa 10 na kisima cha maji viko tayari kwa matumizi.

Waziri pia aliahidi kutoa Sh. milioni tatu kutoka kwenye mfuko wa jimbo kukamilisha ujenzi wa nyumba ya mwalimu ili shule hiyo ipate usajili mapema.

Wananchi wa Misrey walitumia fursa hiyo kueleza kero mbalimbali zinazowakabili ambazo zilitolewa ufafanuzi na wataalamu mbalimbali waliokuwepo kwenye tukio hilo.

Akifanya majumuisho ya tukio la upandaji miti, Dk. Kijaji aliwasihi wananchi kuongeza jitihada za kujiletea maendeleo katika mwaka huu kwa kutumia vizuri fursa zinazotolewa na serikali ikiwamo kujikita kwenye kilimo cha alizeti.





# Watoto wadaiwa kuiba vyombo na kuviuza kama chuma chakavu

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

BAADHI ya watoto wenye umri kati ya miaka 10 na 14, wanadaiwa kujihusisha na biashara ya vyuma chakavu na kuwa chanzo cha wizi wa vifaa vya nyumbani kama sufuria na vyenye asili ya chuma.

Hayo yalisemwa jana na baadhi ya wakazi wa mji wa Vwawa, Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe ambao walidai kuwa kumekuwa na udokozi majumbani mwao wa vifaa kuviuza kwa wafanyabiashara wa chuma chakavu.

Mkazi wa Mtaa wa Ukingani, Helena Mwampashi, alisema umeibuka wizi wa vyombo vya nyumbani na kwamba wezi hao wanavizia, wakikuta zimeanikwa sufuria au sahani za chuma. Hizichukua na kwenda kuziuza.

Naye Lucas George, mkazi wa mtaa wa Ilolo mjini Vwawa, alisema vitendo vya wizi mdogo mdogo wa vyombo vya nyumbani ni wa muda mrefu. Alisema katika eneo lao, kinamama wanaopika pombe wanaibiwa hadi mapipa wanayotumia, sufuria, majiko ya mkaa na vyombo vingine.

"Jana (juzi) tu kuna kijana alikamatwa baada ya kupita gereji ya pikipiki na kuiba 'block' ya pikipiki. Baada ya kupigwa alikubali na kwenda kuonyesha alikouza na kupewa Sh. 2,500. Hata hivyo kijana huyo tulimtambua ni yatima hivyo hata polisi hatukumpeleka," alisema George.

Diwani wa Vwawa, George Kiwaya, alisema wizi wa vyombo vya nyumbani, hasa wa vitu vyenye asili ya chuma, unafanywa na watoto wadogo ambao huiba na kwenda kuwauzia wafanyabiashara wa chuma chakavu.

"Wakishaiba vyombo hivyo wanaviharibu kabla ya kwenda kuuza ili viweze kuuzika. Hali hiyo imetulazimu kufuatilia mienendo ya watoto wetu hasa nyakati ambazo wazazi wako kazini ili tuwadhibiti," alisema Kiwaya. Mmoja wa wafanyabiashara wa chuma chakavu mjini Vwawa, Fudwello Mwampamba, amekiri baadhi ya vyuma vinavyoletwa kuuzwa kwake hasa na watoto wadogo huvitilia shaka na kuwarudisha navyo ili warejeshe walikochukua.

"Tunavitambua vizuri kitu kama sufuria unakuta ina masizi mapya au ina ukoko inaeleweka kwamba ilikuwa ikitumika mahali," alisema Mwampamba.

Mfanyabiashara mwingine, aliyejitambulisha kwa jina la Chisunga, alisema siku za nyuma kulikuwa na malalamiko toka kwa watu kuhusu kupotelewa na vyombo vyao, lakini hali hiyo imepungua siku hizi.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Songwe, Lughano Mbingu, alikiri miundombinu ya madaraja kubomolewa na kuondolewa vyuma.

Hata hivyo, hakuthibitisha moja kwa moja waharibifu hao wanakwenda kufanyia matumizi gani.

Alisema kutokana na uharibifu huo siku hizi wameacha kuweka vyuma kwenye kingo za madaraja na badala yake wanaweka zege.



Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, akiwa kwenye mkutano na wananchi wa Kata ya Itende kwa lengo la kutoa taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Sh. milioni 470 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika kata hiyo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# DC ataka utunzaji vyanzo vya maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Vincent Anney, ameitaka Bodi ya Bonde la Ziwa Nyasa kuimarisha uhusiano mzuri na nchi jirani za Msumbiji, Malawi na Zambia zinazozunguka bonde hilo ili kufanikisha utunzaji wa mazingira kwa kutunza vyanzo vya maji.

Dk. Anney alisema hayo juzi alipozindua mpango wa usimamizi jumuishi na uendelezaji wa rasilimali za maji wa bonde la Ziwa Nyasa uliowashirikisha wadau mbalimbali kutoka mikoa ya Mbeya, Njombe, Songwe na Ruvuma.

Alisema njia pekee ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ni kushirikiana na nchi jirani kwa kuhakikisha watoa elimu kwa wananchi juu ya athari za mabadiliko hayo.

"Tunahitaji kuweka mipango mikakati ya pamoja kwa kushirikisha nchi hizi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanasababishwa uharibu wa mazingira," alisema Dk. Anney.

Mkurugenzi wa Bodi ya Bonde la Ziwa Nyasa, Elice Englebeth, alisema moja ya majukumu yao ni kulinda vyanzo vya maji ili visiharibiwe.

Pia alisema kuna vikwazo vinavyochangia uharibifu wa mazingira ikiwamo shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji na kwamba ili kudhibiti hali hiyo, wanaendelea kuweka mipaka ili kuepuka uvamizi.

Aliongeza kuwa bado wanaendelea na ushirikiano baina ya Tanzania na nchi zingine za kusini mwa jangwa la Sahara kwa kuzingatia mikataba ya kimataifa iliyotiwa saini na mataifa hayo.

Mpango wa usimamizi jumuishi na uendelezaji wa rasilimali za maji wa Bonde la Ziwa Nyasa uliandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wakulima, wafugaji, wavuvi na viongozi wa serikali za mitaa pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali.

## Washauriwa kupanda mazao kuhimili ukame

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WAKULIMA wa Wilaya za Momba na Songwe, wameshauriwa kupanda mazao kama vile maharage na mtama ili kupambana na ukame ambao unaweza kusababisha baa la njaa katika maeneo yao.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Tawala Msaidizi Idara ya Kilimo, Vanscar Kulanga, alipozungumza na wakulima wa wilaya hizo sehemu ya kuwakumbusha msimu mpya wa kilimo.

Alisema miongoni mwa mazao ambayo wanapaswa wakulima wasiyapuuze ni maharage na mtama ambayo kwa kiasi kikubwa yanahimili mabadiliko mbalimbali ya hali ya hewa na yanasaidia kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

Alidai licha ya mvua za masika kuanza kunyesha baadhi ya maeneo lakini ni muhimu kukachukuliwa tahadhari kwa kupata mazao yanayohimili hali yeyote ya hewa kama vile mtama na maharage.

"Hali ya kiangazi inaweza kusababisha baa la njaa katika jamii, mbali na kupanda mazao kama vile mahindi, mpunga lakini mazao kama alizeti, maharage na mtama ambayo yanahimili hali zozote za hewa ni muhimu yakapandwa," alisema Kulanga.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha msimu huu wa kilimo wakulima wanapata taarifa sahihi za kupanda mazao na matumizi sahihi ya pembejeo na kuwasisitiza maofisa ugani katika kila kijiji kuwatembelea ili kuwapatia elimu ya kilimo bora.

Athuman Kalago, mmoja wa wakulima katika kijiji cha Kilimampimbi, alisema kukosekana kwa mvua za uhakika katika ukanda huo kumesababisha hofu kwa jamii kwamba ni lini wataanza kupanda mazao yao.

Pia aliwasisitiza wakulima wenzake kuendelea kufuatilia taarifa za utabiri wa hali ya hewa ili kujua ni lini muda sahihi wa kupanda mazao yao pamoja na kuzingatia ushauri wa wataalamu wa maofisa ugani.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, aliwataka wananchi kutouza chakula chote kutokana na tishio la ukame.

**Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, aliwataka wananchi kutouza chakula chote kutokana na tishio la ukame.**



# Waziri aeleza umuhimu wa uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohammed, amesema uchumi wa bluu utaokoa nchi.

Amesema kwa sababu Zanzibar ina bahari na endapo samaki watavuliwa kwa usahihi, uchumi wa nchi utaimarika.

Dk. Khalid alisema hayo jana wakati akizindua uvuvi wa bahari kuu kwa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) Makao Makuu ya Kikosi hicho, Kibweni nje ya Zanzibar.

Alisema Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi anasisitiza kutumia rasilimali zilizopo na rasilimali kubwa iliyo nayo Zanzibar ni bahari ambayo bado haijatumiwa kikamilifu ndiyo maana amekuja na dhana ya uchumi wa bluu.

Katika uchumi wa bluu, alisema kuna bahari ndani yake na kuna samaki, hivyo wakivuliwa kwa weledi kutasaidia kupata matumizi na kusafirisha nje ya nchi.

Alisema baharini kuna rasilimali ya mafuta na gesi ambayo inachangia ukuaji wa uchumi, kuna usafiri na usafirishaji na sekta hiyo ikitumiwa inavyostahili ina mchango mkubwa katika pato la taifa, ukuaji uchumi na ustawi wa jamii.

"Baharini kuna madini mbalimbali. Baharini tunaweza tukalima, majongoo, samaki, tukafuga kaa tutawapatia wananchi kipato na fursa za kujikimu kiuchumi," alisema.

Alisema Rais Dk. Mwinyi amekuja na muono mkubwa zaidi wa kuvitumia visiwa vidogo vilivyoko Zanzibar kwa ajili ya kutumika kwa manufaa ya wananchi ndiyo maana serikali imevikodisha kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya utalii.Katika kuwekeza kwenye visiwa hivyo, alisema KMKM ina nafasi kubwa katika suala la usalama na kukabiliana na majanga endapo ajali itatokea.

Pia alisema kikosi hicho kina kazi kubwa tatu ya kwanza ikiwa ulinzi na serikali imekiwezesha kwa vifaa vya kisasa zikiwamo boti za doria.

Alisema kazi ya pili ya kikosi hicho ni uokozi na askari wake wamepatiwa mafunzo na serikali inawategemea katika suala hilo.

"Sisi tumezungukwa na kisiwa na watu wetu wanafanya shughuli za kiuchumi baharini, lakini vilevile usafiri wetu ni wa baharini kwa hivyo mmejipanga zaidi katika suala la uokozi ambayo ni kazi yenu. Hongereni sana kwa mlivyojipanga," alisema.

Kazi ya tatu, alisema ni kujipanga katika kuwekeza na kwamba vikosi vyote vya ulinzi duniani, vinafanya kazi ya uwekezaji katika nchi na hiyo ina faida kubwa ikiwamo kikosi kujilinda kiuchumi na kuwa na fedha ya kujiendesha na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Waziri huyo alikipongeza kikosi hicho katika kushiriki kwenye kuwekeza kiuchumi ikiwamo masuala ya uvuvi katika bahari kuu.



Mkuu wa Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), Komodoo Azan Hassan Msingiri (wapili kushoto), akiwa na wapiganaji wa kikosi hicho akionyesha samaki mwenye uzito wa kilo 90 ambaye kwa soko la kimataifa huuzwa kwa Sh. 990,000 baada ya kufanikiwa kuvua tani tatu, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Waziri aeleza mageuzi elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema kabla ya Mapinduzi, Zanzibar ilikuwa ina shule 62 za msingi zilizoandikisha wanafunzi 24,334 lakini kwa sasa imeongezeka na kufikia 545 zilikuwa na wanafunzi 331,425 kwa Unguja na Pemba.

Pia amesema kabla ya Mapinduzi elimu ilikuwa ikitolewa kwa ubaguzi lakini kwa jitihada za Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume, sasa inapatikana bure kwa wananchi wote.

Waziri Saada aliyasema hayo jana wakati akifungua madarasa mapya manane ya Shule ya Maandalizi na Msingi Binguni, Kusini Unguja ambayo yatapunguza msongamano wa wanafunzi.

Alisema serikali inaweka msingi wa maendeleo katika elimu kwa kuweka miundombinu bora kwa wanafunzi ili kuhakikisha wanapata elimu bora.

Pia alisema serikali itahakikisha inaendelea kuimarisha sekta ya elimu ili miundombinu yake iimarike na kuhakikisha fursa ya elimu haiwapiti watoto.

Waziri Saada alibainisha kwamba serikali inaweka jitihada za kuweka miundombinu ya elimu ili kutoa ari kwa wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani yao ya taifa na kuiomba ofisi ya wilaya kuhakikisha shule hiyo inafanya vizuri katika matokeo.

Aliipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kufanya mageuzi makubwa katika sekta hiyo, ikiwamo kurudisha darasa la saba ili kuwafanya wanafunzi kukaa shuleni na kupata uelewa mzuri wa kufanya vizuri katika masomo yao hasa mitihani yao ya taifa.

Waziri aliwashauri wazazi na walezi kuwasimamia watoto wao kimasomo na kimazingira ili kuwakinga na matendo mabaya ya udhalilishaji yaliyoshika kasi.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis Juma, alisema wamepiga hatua kubwa katika upatikanaji wa elimu na awali shule hiyo ilikuwa na madarasa machache hali ambayo ilisababisha kuwa na msongamano mkubwa wa wanafunzi madarasani.

# Mwinyi atuma salamu rambirambi kwa ndugu waliofariki ajali ya boti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametoa salamu za rambirambi kwa familia za watu waliofariki dunia kutokana na ajali ya kuzama kwa boti mkoa wa Kusini Pemba.

Ajali hiyo iliyotokea Kisiwa Panza, Pemba ilisababisha watu 10 kati ya 30 waliokuwamo katika boti hiyo kufariki dunia.

Katika salamu hizo za rambirambi, Rais Dk. Mwinyi alieleza kusikitishwa na vifo hivyo na kuzinasihi familia za marehemu hao kuwa na subira na ustahamilivu katika kipindi hiki kigumu.

Ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 10:00 jioni baada ya boti waliyokuwa wakisafiria wananchi hao kwenda msibani Kisiwa Panza wakitokea Chakechake kuzama.

Kisiwa Panza ni moja ya visiwa vidogo tisa vinavyoishi watu Zanzibar na hujishughulisha na mambo mbalimbali yakiwamo ya kiuchumi na kijamii.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Mkoani Pemba, Khatib Juma Mjaja, watu tisa wakiwa wameshafariki dunia, miili yao iliopolewa mapema baada ya ajali na mmoja alipatikana usiku wa kuamkia jana.

Alisema pia watu 15 wameokolewa wakiwa hai na kuruhusiwa kurudi majumbani wakiwa na hali nzuri kiafya.

"Tumebahatika kuwaokowa watu 15 wakiwa hai na maiti 10 za wasafiri hao ambao tayari walishakabidhiwa kwa jamaa zao kwa mazishi ingawa juhudi za uokozi zinaendelea," alisema.

Mjaja aliwataka wananchi ambao wana jamaa zao wanadhani waliingia kwenye boti hiyo na hawajawaona mpaka sasa, waripoti katika vyombo husika ili kuendelea kutafutwa ili wajulikane kuwa wako hai au

wamefariki dunia.

Alisema serikali ya wilaya iko pamoja na wale wote waliokumbwa na msiba huo katika kipindi hiki cha maombolezo.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mkoani Pemba, Mohammed Faki Saleh, alithibitisha kupokewa kwa maiti 10 na majeruhi 15 wa ajali hiyo.

Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Omar Machano (50), Rashid Hamad (30), Suleiman Hamad (32), Moh'd Soud, Nassor Issa Omar (34) na Salim Juma Said (55).

Wengine ni Ali Makame Shehe, Shasha Khamis Abdalla, Hassan Mati Haji (22) na Idrisa Omar Aley.

Waliokolewa wakiwa hai ni Hamad Omar Mselem, Bambi,

Khamis Ali Khator, Khalifa Moh'd Abdalla, Khamis Yussuf Moh'd, Haji Muhamad, Omar Jibran , Ali Shehe Othman, Suleiman Jibran, Bakar Salim Jibran, Suleiman Juma Moh'd, Shaaban Ali Hamad, Suleiman Moh'd Khamis, Haji Moh'd Juma na Abdalla Kassim Moh'd.

Kamanda wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), Komodore Azan Msingiri, alisema wameshapeleka wazamiaji 12 ambao wako baharini kuangalia kama kuna watu waliobakia wakiwa hai au kufariki dunia.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA ……149….2021**
**MDAI: FREDY WILBROAD KAYOMBO**
**MDAIWA: SUSAN WARREN BALAIGWE**
**Kwa: SUSAN WARREN BALAIGWE**
**Ombi la mdai: Fredy wilbroad kayombo**
**Madai ya :pesa sh.4,000,000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo tarehe 10 mwezi 01 mwaka 2022 saa8:30 asubuhi.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 14 mwezi 12 mwaka 2021.

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP.117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED.I ANTONIA RAYMONDI MASSAWE P.O. BOX 3041 MOSHI** with mobile phone **0758594166**, formerly known as **ANTONIA MKAHATARI MASSAWE**, a national and citizen of United Republic of Tanzania by birth **DO HEREBY ABSOLUTELY RENOUNCE AND ABANDON** the use of my former names as above and in lieu thereof do assume as from the date hereof my new name of **ANTONIA RAYMONDI MASSAWE**
**AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUEST** all persons at all times hereafter to designate and address me by such assumed name of **ANTONIA RAYMONDI MASSAWE** only and not my former names.

**SIGNED** and **DELIVERED** at MOSHI by the said **ANTONIA RAYMONDI MASSAWE** Who is known to me personally/identified to me by…… the latter being known to me personally in my presence this 13 day of December, 2021. ……………………………………

**DEPONET**

**BEFORE ME: -**
**NAME……………………………**
**ADDRESS: …………………………**
**SIGNATURE…………………………**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

SIRIAMANI CORNEL MFOY
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari, Yenye namba za usajili T 901DSQ
Chassis namba ZZE122-3046514, Engine namba 1ZZ-1134192
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi Taarifa:
KIL/MOS/RB/3248/2022

**(CAP 117 R.E. 2002)**
**DEED POLL**



**I , YASINTA ANACRETH EMMANUEL,** of P.O. Box …………….**MWANZA DO HEREBY** absolutely renounce and abandon the use of my former names of YASINTA MARCEL EMANUEL and in lieu thereof do hereby assume the names of YASINTA ANACRETH EMMANUEL.
The reason for s un change is that during citizenship registration with the National Identification Authority (NIDA) my middle name was wrongly written as MARCEL which in fact is the name of my Grandfather, my correct middle name is ANACRETH which is the first name of my father. Further, the name EMANUEL is simply a spelling error, the correct spelling is EMMANUEL
AND IN PURSUANCE of such change of my names as aforesaid I hereby declare that I shall at all times hereinafter and in all records, deed and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use the said assumed names of **YASINTA ANACRETH EMMANUEL** as my names in lieu of said former names of **YASINTA MARCEL EMANUEL.**
**AND I HEREBY** authorize and request all persons to refer and address me by such assumed names of YASINTA ANACRETH EMMANUEL.
SIGNED and DELIVED at MWANZA
By the said YASINTA ANACRETH EMMANUEL
Who has been identified to me by……………
ANACRETH EMMANUEL the letter being DEPONENT
Known to me personally
This 13.day of December,.2021

**BEFORE ME**
**NAME: MORICE H MTOI**
**SIGNATURE: …………………………**
**POSTAL ADDRESS: 331 MWANZA**
**QUALIFICATION: STATE ATTORNEY**

FOMU MIRATHI - 2
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 10/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MASOUD RASHID BENG'IWA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA KASHINDI YUSUPH MSUMARI**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 01 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 4 Mwezi 01 Mwaka 2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa wa Njombe**
**Usimamiz wa Mirathi Na. 35/2021**
**Katika Shauri la Mirathi ya**
**John Luka Komba…………………………Marehemu**
**Wa Melinze-Njombe**
**Katika shauri la maombi ya kuziba nafasi ya Msimamizi**
**Aliyefariki yaliyoletwa na**
**Bahati Luka Komba…………………Mwombaji**
**TANGAZO KWA UMMA**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14 Mwezi 01 Mwaka 2022 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu Maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
Zingatia: Endapo kuna yeyote mwenye au anayejua kuhusu uliko wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 03 Mwezi 01 Mwaka 2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TANZANIA**
**HATI YA KIAPO**

Mimi SHABBIR HUSSEIN MOIZALI wa Tanga, Muislam, mtu mzima na akili zangu timamu bila ya kushawishiwa na mtu yeyote naapa kama ifuatavyo:-

- KWAMBA, mimi SHABBIR HUSSEIN MOIZALI ni mmiliki wa gari aina ya NOAH T.956 CQX.
- KWAMBA, kadi ya umiliki wa gari hilo imepotea na uwezekano wa kupatikana hakuna tena na nimetoa taarifa polisi na kupatiwa Loss Report Na. TAN/RB/4907/2022.
- KWAMBA, kwa kiapo hiki naiomba Idara husika itambue kuwa mimi SHABBIR HUSSEIN MOIZALI sina kadi ya umiliki wa gari hilo.

**UTHIBITISHO**
Mimi SHABBIR HUSSEIN MOIZALI, nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kuanzia aya ya 1-3 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sheria ya viapo (The Oaths and Statutory Declaration Act.Cap.34 R.E 2002)

SHABBIR HUSSEIN MOIZALI

**MBELE YA…A.KHAMISI**
**CHEO…HAKIMU MKAZI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi……02..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NASSORO ISSA MAHAMBA WA MKOMOLA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA TATU NASSORO MAHAMBA.**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 13/01/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 05/01/2022**

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA



## Bobi Wine ampa neno Museveni katika mashairi

**Kampala,** UGANDA

KIONGOZI wa upinzani Uganda na mwanamuziki Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine, ameachia wimbo mpya kwa jina Ogenda, neno la Kiganda linalomaanisha 'Utaanguka'.

"Wimbo huo unamlenga Rais Yoweri Museveni moja kwa moja, kwa sababu ya kukiuka ahadi yake kuleta demokrasia nchini," anasema Bobi Wine.

Bobi Wine ameiambia BBC kwamba, alilazimika kufichua uhalifu uliofanywa chini ya utawala wa rais, na sababu picha zilizotumika kwenye video kuwa za kutisha.

"Utawala nchini Uganda umewekeza pesa nyingi kuficha ukatili huo," alisema.

Bobi Wine alisema vyombo vya habari, Uganda, vimezimwa na kwamba, njia pekee ya kufichua uozo huo ni kupitia muziki.

"Haki inaweza kupatikana pale tu tunapofichua uhalifu, ndiyo maana tunaendelea kuuibua, hiyo ndiyo njia pekee tunayoweza kupambana nayo," alisema.

**BBC**

## Waziri Mambo ya Nje China kuzuru Kenya

**Nairobi,** KENYA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, amewasili Eritrea, juzi katika kituo cha kwanza katika ziara ya mataifa matatu barani Afrika ambayo pia itakwenda Kenya na Comoro.

Waziri wa Habari wa Eritrea, Yemane Meskel, katika chapisho kwenye Twitter, alisema kuwa Wang alipokelewa na Waziri wa Mambo ya Nje, Osman Saleh na maofisa wengine wakuu katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Asmara.

Yemane alisema, Wang atakuwa nchini humo kwa siku mbili na atafanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje na baadaye Rais Isaias Afwerki.

China, imeongeza juhudi za kutumia misaada ya chanjo ya Covid-19, ili kuimarisha ushawishi wake barani Afrika, huku kukiwa na onyo jipya kutoka Marekani kwa washirika wa Kiafrika, kuhusu kile kinachoitwa diplomasia ya mtego wa deni.

**BBC**

# Vital Kamerhe kutibiwa nje ya nchi

**Kinshasa,** DRC

MKURUGENZI wa zamani katika ofisi ya Rais Felix Tshisekedi, Vital Kamerhe yuko huru tangu Desemba 6, mwaka jana, kufuatia hatua ya kuachiliwa kwa muda.

Vital Kamerhe, sasa ameruhusiwa kuondoka DRC. Aliondoka na kwenda Ulaya, juzi, jioni.

Kulingana na Billy Kambale, katibu mkuu wa chama wa UNC, hatua hiyo imechukuliwa kwa sababu za kiafya.

Vital Kamerhe alihukumiwa kifungo cha miaka 13 jela kwa ubadhirifu wa fedha za umma.

Hakuna chanzo kinachozungumzia suala hilo kwa uwazi, wasaidizi wake wakihofia kwamba huenda mambo yakabadilika katika dakika za mwisho.

Ndani ya chama chake cha kisiasa na familia yake, wote wanabaini kwamba mkurugenzi mkuu wa zamani katika ofisi ya Felix Tshisekedi, bado ana wapinzani wengi.

"Hatutaki kuwapa faida kwa wale ambao wanaweza kudidimiza mambo. Tunataka kumlinda kiongozi wetu," mmoja wa washirika wake wa karibu aliiambia RFI.

Operesheni ya kumsafirisha ilifanywa kwa uangalifu na kwa siri kubwa. Inajulikana tu kuwa alienda Ulaya, aliokwenda bado ni siri kwa sasa.

Kulingana na vyanzo kutoka chama chake, watu watatu waliandamana naye: katibu wake, mkewe na daktari wake.

Ndugu zake wanasema, amekuwa akilalamika kuhusu matatizo ya kupumua kwa miezi kadhaa.

Tayari kabla ya kuachiliwa kwake kwa muda, Vital Kamerhe, hakuwa tena kizuizini katika gereza kuu la Makala.

Aliwekwa ndani katika kituo cha matibabu katika mji mkuu.

Kwa wakati huu, hakuna tarehe ya kurudi kwake nchini ambayo imetangazwa.

Wasaidizi wake wanabainisha kuwa kibali cha kuondoka alichopewa hakitaji maelezo hayo.

**RFI**



Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi (wapili kulia), akiwasili nchini Eritrea na kupokelewa na mwenyeji wake, Waziri wa Habari, Yemane Meskel, juzi. **PICHA: BBC**

## Ripoti: Zuma alihusika na ufisadi

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

TUME iliyokuwa inachunguza visa vya ufisadi wakati wa uongozi wa aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, imetoa sehemu ya ripoti yake baada ya miaka mitatu.

Tume hiyo iliyoongozwa na Jaji Raymond Zondo, iliundwa mwaka 2018 kuchunguza na kubaini visa vya ufisadi wakati wa uongozi wa Rais Zuma, aliyekuwa madarakani kwa miaka tisa tangu mwaka 2009.

Baada ya mashahidi zaidi ya 300 kuhojiwa, tume hiyo ilielezea kuhusu wizi wa fedha za umma ulivyofanyika katika Shirika la ndege la Afrika Kusini, pia uhusiano wa karibu wa wafanyabiashara maarufu Atul, Ajay na Rajesh Gupta, ambao walikuwa wanapata mikataba mbalimbali na serikali.

Hata hivyo, Zuma ameendelea kukanusha madai ya kuhusika na visa vya ufisadi na hata alikataa kutoa ushirikiano na tume hiyo na kusababisha kufungwa jela kwa kukaidi agizo la mahakama.

Katika mapendekezo yake, tume hiyo inataka serikali kuja na mbinu za kupambana na ufisadi katika eneo la manunuzi, serikalini, kuwalinda wanaofichukua wizi wa fedha za umma na kuundwa kwa tume huru ya kupambana na ufisadi.

**RFI**

## Tembo aua mama na mwana

**Harare,** ZIMBABWE

MAMA na mtoto wake wa miezi kadhaa, wamekanyagwa hadi kufa na tembo Kusini-Mashariki mwa Zimbabwe.

Mwanamke huyo, ambaye alikuwa amewatembelea jamaa zake katika Wilaya ya Chipinge vijijini, wakati wa sikukuu ya Mwaka Mpya, alikuwa njiani kurudi nyumbani tembo alipowashambulia.

Msemaji wa Mamlaka ya Hifadhi za Zimbabwe, Tinashe Farawo, alisema kuwa tembo huyo aliwashambulia ghafla na kuwaua wawili hao papo hapo, lakini tembo huyo aliuawa.

**BBC**

HABARI MICHEZO

# YANGA YATANGAZA JEMBE JIPYA USIKU, BADO MMOJA

**Na Adam Fungamwangwo**

WAKATI ikikamilisha usajili wa mchezaji mpya juzi usiku, Crispin Ngushi, kutoka Mbeya Kwanza FC, mabosi wa Yanga wamesema bado imebaki nafasi moja ya kusajili nyota mpya katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

**Mabosi hao wa Yanga wamesema usajili huo uliobakia utakuwa ni wa mwisho kwa klabu yao kwa sasa.**

Yanga imemtambulisha straika huyo mpya ambaye mpaka sasa amefunga mabao matatu kwenye Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ambayo imesimama kwa muda kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayofanyika huko Zanzibar.

"Crispin Ngushi sasa ni kijani na njano." Iliandikwa katika mtandao wa klabu hiyo, ikimtambulisha usiku mkubwa.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, amesisitiza mchezaji huyo ni wa nne kusajiliwa na klabu hiyo, hivyo kuna mwingine wa mwisho ambaye anaweza kutangazwa leo au kesho na atafunga dimba la usajili huu wa dirisha dogo.

"Kama nilivyosema huko nyuma kuwa kocha wetu alihitaji wachezaji wanne au watano kwenye kipindi hiki cha usajili. Jana (juzi), tumeshusha kitu na tumekitangaza usiku, sisi kila siku tunakuja na staili mpya ya kutambulisha wachezaji wetu. Sasa kesho (leo) au keshokutwa (kesho), tunaweza kutangaza mchezaji mwingine. Huyo atakuwa wa mwisho na ndiyo atafunga dimba kwenye dirisha letu la usajili," alisema Bumbuli.

Tayari Yanga imetimiza jumla ya wachezaji wanne iliyowasajili kwenye kipindi kifupi tu cha dirisha dogo la usajili, huku wote wakiwa ni wazawa.

Ilianza kwa kumsajili kiungo mshambuliaji, Salum Aboubakar kutoka Azam FC, kabla ya kumsajili kipa, Aboutwalib Mshery aliyekuwa Mtibwa Sugar na baadaye akafuatia winga, Dennis Nkane kutoka Biashara United.

Dirisha dogo la usajili litafungwa rasmi ifikapo Januari 15, mwaka huu na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limesisitiza hakutakuwa na muda wa nyongeza kwenye mchakato huo ambao unafanyika kwa njia ya mtandao.

# *DStv yatambulisha Panda Tukupandishe*

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 2022 unaanza na habari njema kwa wateja wa DStv baada ya kuanza kwa promosheni yake kabambe ijulikanayo kama 'Panda Tukupandishe' ambapo wateja watapatiwa vifurushi vya juu ili kufurahia zaidi burudani katika kipindi hiki cha mwanzo wa mwaka.

Promosheni hii itadumu kwa miezi mitatu na ni kwa wateja wa vifurushi vya DStv Poa, Bomba, Shangwe na Compact. Akitangaza promosheni hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Uhifadhi Wateja wa MultiChoice Tanzania, Hilda Nakajumo, amesema katika promosheni hiyo, mteja wa DStv atakayelipia kifurushi cha juu ya kile anachotumia atapandishwa na kupewa kifurushi cha juu zaidi kwa mwezi mmoja bila gharama za ziada.

"Mathalan, mteja wa DStv Poa (Sh 9,900) akilipia kifurushi cha juu yake ambacho ni DStv Bomba (Sh. 21,000) atapandishwa na kupewa kifurushi cha DStv Shangwe (Sh. 31,000) chenye chaneli zaidi ya 100," alisema Nakajumo.

Aliongeza mteja wa kifurushi cha Shangwe, akilipia kifurushi cha Compact atapandishwa na kupatiwa kifurushi cha Compact Plus chenye chaneli zaidi ya 140, huku mteja wa kifurushi cha Compact akilipia Compact Plus atapewa kifurushi cha juu kabisa cha DStv Premium chenye chaneli zaidi ya 150.

"Tungependa kuona wateja wetu wakiendelea kupata burudani kipindi hiki cha mwanzo wa mwaka ambacho kinafahamika kwa kuwa na majukumu mengi. Promosheni hii inawawezesha wateja wetu kupata habari, burudani na elimu zaidi kwa kupata vifurushi vya juu vyenye chaneli nyingi zaidi. Tunaamini hii ni zawadi nzuri ya mwaka mpya kwa wateja wetu na tunaamini wataifurahia," alisema ofisa huyo.




Ofisa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Shumbana Walwa (kushoto), akimtambulisha mmoja kati ya wachambuzi mahiri wa soka nchini, Ibrahim Masoud 'Maestro' katika uzinduzi wa kampeni ya Panda Tukupandishe iliyofanyika katika makao makuu ya kampuni yao jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Azam FC yaipigia hesabu Namungo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kupata ushindi katika mechi yake ya kwanza, Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdulhimid Mohamed, amesema kikosi chake kimejipanga kupambana katika mechi dhidi ya Namungo ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Azam FC ilipata ushindi wa bao 1-0 katika mechi yake ya kwanza dhidi ya Meli 4 City hapo juzi, mfungaji akiwa ni Shabani Chilunda katika dakika ya 17.

Abdulhimid alianza kwa kuwapongeza wachezaji wake kwa kazi nzuri waliyofanya na kuongeza anaamini wataendelea kufanya vyema katika michezo inayofuata.

"Mashindano haya ni magumu na wala si ya kuyafanyia masihara, licha ya ratiba kubana lakini nitahakikisha timu inapata matokeo mazuri ili tuvuke hatua hii ya makundi salama," alisema Abdulhimid.

Hata hivyo kocha huyo alisema ana wasiwasi kama mshambuliaji wake, Chilunda aliyepata majeraha juzi kama mechi ya leo anaweza kumjumuisha.

## Tshishimbi, Chinedu rasmi Kitayosce

**Na Adam Fungamwangwo**

KIUNGO mkabaji wa zamani wa Yanga, Papy Tshishimbi na aliyekuwa straika wa Biashara United na Alliance FC, Michael Chinedu, wamejiunga na Kitayosce ya Tabora ambayo inashiriki Ligi ya Championship, imefahamika.

Kocha Mkuu wa Kitayosce, Fulgence Novatus, aliliambia gazeti hili usajili wa wachezaji hao umeshakamilisha na wanaamini lengo la kukiongezea kikosi chao nguvu litatimia.

Fulgence alisema wanaendelea kujiimarisha kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vyema kwenye ligi hiyo na hatimaye wanapanda daraja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Tumekamilisha usajili wa wachezaji wawili ambao ni kiungo Mkongomani Papy Kabamba Tshishimbi na Michael Chinedu, ni usajili mzuri nadhani utatusaidia kwenye harakati zetu," alisema Fulgence.

Tshishimbi aliichezea Yanga kuanzia mwaka 2018 hadi 2020, alipoamua kuondoka na kujiunga na AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**AUBAMEYANG RASMI SOKONI**

ARSENAL itapokea ofa ya mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 32, ambaye anaweza kuondoka katika klabu hiyo mwezi huu. ***(Sky Sports)***

**VLAHOVIC KUTUA ARSENAL**

ARSENAL wametangaza ofa ya euro milioni 70 kumnunua mshambuliaji wa Fiorentina na Serbia, Dusan Vlahovic - hatua ambayo huenda ikamfanya kiungo wa kati wa Uruguay, Lucas Torreira, 25, kuhamia klabu hiyo kwa mkataba wa kudumu. ***(Gazzetta dello Sport)***

**ADEYEMI KUMRITHI HAALAND**

MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg, Karim Adeyemi, 19, analengwa na Borussia Dortmund kuchukua nafasi ya mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland (21). ***(Marca)***

**HATIMA YA HAALAND**

KLABU ya Borussia Dortmund inataka hatima ya Erling Haaland kuamuliwa kabla dirisha la uhamisho wa Januari kufungwa. ***(Mirror)***

**BARBOSA AITAKA NEWCASTLE**

MSHAMBULIAJI wa Flamengo, Mbrazil Gabriel Barbosa, 25, yuko tayari kujiunga na Newcastle United licha ya klabu hiyo kukabiliwa na tishio la kushuka daraja. ***(90min)***

**DE BEEK NJIA MOJA**

KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek, 24, atatathmini chaguo lake Januari huku mchezaji huyo akifikiria kuondoka Manchester United. ***(ESPN)***

**SPURS YAZIDI KUJIPANGA**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte bado hajakutana na Mwenyekiti, Daniel Levy, kujadili uhamisho wa Januari. Kiungo wa kati wa AC Milan na Ivory Coast, Franck Kessie, 25 ni miongoni mwa wachezaji wanaolengwa na Mtaliano huyo. ***(Evening Standard)***

**NKETIAH AWANIWA**

KLABU za Brighton na Crystal Palace zinapania kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah, 22, Januari hii. ***(Sun)***

**MAITLAND- NILES SAFI**

AS Roma inajiandaa kukamilisha uhamisho wa mkopo wa kiungo wa kati wa Arsenal, Ainsley Maitland-Niles, 24 wiki hii. ***(ESPN)***

**PSG YAMTAKA DEMBELE**

KLABU ya Paris St-Germain wanapanga kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Ousmane Dembele, 24. ***(Mundo Deportivo)***

**BARCA YAMTEGA DEMBELE**

BARCELONA itamuuza, Ousmane Dembele endapo winga huyo atakataa ofa ya mwisho ya mkataba mpya. ***(Talksport)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TUCHEL AENDELEA KUMCHUNIA LUKAKU

### Asema hatabadilisha mfumo wa kikosi chake na kumtaka mshambuliaji huyo...

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amekataa kubadilisha staili ya uchezaji ili 'kumfiti' straika, Romelu Lukaku na kusisitiza "hatuwezi kucheza kama Inter".

**Lukaku aliibua mjadala mkubwa baada ya mahojiano yake ya Alhamisi na Ijumaa kuelezea namna ambavyo hana furaha kwa hali ya sasa ilivyo dani ya kikosi cha Chelsea.**

Pia alibainisha uhusiano wake mzuri na kocha, Antonio Conte, ambaye alifanya nae kazi Inter, wakati akielezea angependa kurudi kucheza kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, siku moja.

Tuchel alimwadhibu Lukaku kwa kauli yake hiyo kwa kutomjumuisha kwenye kikosi kilichocheza dhidi ya Liverpool kabla ya wawili hao kuwa na mazungumzo Jumatatu na walionekana kama walemalimaliza suala hilo.

Halafu Lukaku akajitokeza hadharani kuomba msamaha kwa mashabiki wa Chelsea kwa kile kilichotokea na ilionekana kama Tuchel ametulia, lakini raia huyo wa Ujerumani amesisitiza hatabadilisha staili ya uchezaji ya kikosi chake kwa ajili tu ya fowadi huyo.

Alipoulizwa kuhusu kauli ya Lukaku kwa Conte na staili ya uchezaji ya Chelsea, Tuchel alisema: "Inafanya kazi kwa njia zote na tunafanya hivyo kwa kila mchezaji, sisi tuna mfumo fulani na misingi yetu ya namna gani ya kucheza.

"Nahisi yeye anatakiwa kuwa mtulivu kuliko kitu kingine chochote, anataka kuhusika sana na kuwa na nafasi kubwa.

"Ni ngumu kwake kukubali hali kama hiyo muda mwingine."




CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 823



# MORATA, DE LIGT WAPEWA DARASA

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Miralem Pjanic, amewaonya, Alvaro Morata na Matthijs de Ligt, kufikiria kwa makini kabla ya kuamua kujiunga na klabu hiyo ya Katalunya.

Morata kwa sasa anacheza kwa mkopo Juventus akitokea Atletico Madrid, lakini ripoti zinadai, kocha mpya wa Blaugrana hao, Xavi anataka kuimarisha safu yake ya ushambuliaji na tayari amempata, Ferran Torres.

Barca haiwezi kukamilisha usajili wa Torres, au mwingine wowote hadi wauze wachezaji wengine kutokana na matatizo ya kifedha, ingawa wamekuwa wakihusishwa na nyota kadhaa.

Rais wa klabu hiyo, Joan Laporta, aliiambia dunia kuwa miamba hao wa LaLiga wanaweza kurudi kwenye ubora wao na kusajili wachezaji wakubwa na wamekuwa wakihusishwa na usajili wa Erling Haaland.

Hata hivyo, Pjanic, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo katika klabu ya Besiktas, amewataka wachezaji wanaofikiria kujiunga na klabu hiyo kuongeza umakini.

Aliiambia Tuttosport: "Morata amekuwa na muda wa kuvutia kwenye uchezaji wake hadi sasa. Amezichezea klabu kubwa kama Chelsea, Atletico Madrid na Juventus.

# Trippier rasmi mali ya Newcastle United

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle imefikia makubaliano ya ada ya pauni milioni 12 ya kumsajili mlinzi wa pembeni wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya England, Kieran Trippier.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 anatarajia kuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa Newcastle chini ya wamiliki wapya wa klabu hiyo kutoka Saudi Arabia na wa kwanza kwa kocha, Eddie Howe, aliyetua hapo Novemba mwaka jana.

Trippier, ambaye alijiunga na miamba hao wa LaLiga, Atletico mwaka 2019 kutoka Tottenham kwa pauni milioni 20, jana Jumatano alitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya yake.

Ataungana na Howe, ambaye alimsajili wakati akiwa kwenye timu ya Burnley.

Trippier amecheza mechi 83 kwa klabu hiyo ya Hispania, ambao walishinda LaLiga msimu uliopita.

Mlinzi huyo alikuwa sehemu ya kikosi cha England ambacho kilifika fainali ya Euro 2020 kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Newcastle wanashika nafasi ya pili kutoka chini kwenye Ligi Kuu England, ikiwa imeshinda mchezo mmoja kwenye mashindano yote.



# 3,998,440

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII
**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 9/1/22 | 16:30 | Cagliari vs Bologna | 3.15 | 3.30 | 2.27 |
| 2. 9/1/22 | 16:30 | Torino vs Fiorentina | 2.56 | 3.41 | 2.66 |
| 3. 9/1/22 | 17:00 | Clermont Foot vs Reims | 2.42 | 3.14 | 2.99 |
| 4. 9/1/22 | 17:30 | Hertha BSC vs FC Koln | 2.66 | 3.46 | 2.51 |
| 5. 9/1/22 | 19:05 | Nantes vs Monaco | 3.22 | 3.27 | 2.23 |
| 6. 9/1/22 | 20:15 | Malaga vs Sporting Gijon | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 7. 9/1/22 | 20:30 | Alaves vs Athletic Bilbao | 3.25 | 3.05 | 2.35 |
| 8. 9/1/22 | 20:30 | Roma vs Juventus | 3.07 | 3.31 | 2.31 |
| 9. 9/1/22 | 20:30 | Genoa vs Spezia | 2.28 | 3.29 | 3.14 |
| 10. 9/1/22 | 22:30 | Ponferradina vs Zaragoza | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 11. 9/1/22 | 23:00 | Villarreal vs Atletico Madrid | 2.84 | 3.19 | 2.54 |
| 12. 9/1/22 | 23:30 | Las Palmas UD vs Almeria | 2.76 | 3.05 | 2.56 |
| 13. 9/1/22 | 23:30 | Belenenses vs FC Arouca | 2.57 | 3.02 | 2.82 |

## MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

**ALHAMISI - 06 - JANUARI 2022**

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5636 | Cuarte CD vs CD Carinena | 1.56 | 4.00 | 6.00 |
| 14:00 | 5656 | Robres CD vs Calamocha | 1.82 | 3.24 | 4.16 |
| 14:00 | 5885 | UD Son Veri vs Ibiza San Rafel | 3.07 | 3.02 | 2.25 |
| 14:00 | 5929 | Felanitx vs CF Soller | 3.14 | 2.94 | 2.27 |
| 14:30 | 3195 | Bologna vs Inter | 5.60 | 4.40 | 1.53 |
| 14:30 | 4534 | Sampdoria vs Cagliari | 1.82 | 3.75 | 4.10 |
| 16:30 | 2004 | Psis Semarang vs Persija Jakarta | 3.03 | 3.22 | 2.17 |
| 16:30 | 4146 | Lazio vs Empoli | 1.61 | 4.40 | 4.71 |
| 16:30 | 5700 | Spezia vs Verona | 2.90 | 3.35 | 2.40 |
| 17:00 | 2817 | Uniao Sao Joao EC SP U20 vs Taquarussu EC TO U20 | 2.75 | 3.37 | 2.27 |
| 17:00 | 3162 | Jamshedpur vs Northeast United FC | 1.84 | 3.52 | 3.66 |
| 17:30 | 4831 | CE Mercadal vs UD Rotlet Molinar | 1.99 | 3.23 | 3.47 |
| 17:35 | 3156 | Yarmouk vs AL Arabi | 9.66 | 6.18 | 1.20 |
| 18:00 | 1317 | ED Moratalaz vs AD Complutense Alcala | 1.75 | 3.23 | 4.53 |
| 18:00 | 1710 | SD Sofan vs Silva SD | 4.23 | 3.13 | 1.84 |
| 18:00 | 3239 | Fuenlabrada vs Cadiz CF | 2.67 | 3.01 | 2.72 |
| 18:00 | 3353 | CD Torrijos vs CD Illescas | 2.23 | 2.98 | 3.17 |
| 18:00 | 4727 | Atletico San Luis U20 vs Pachuca U20 | 1.96 | 3.37 | 3.42 |
| 18:00 | 5323 | Girona vs Osasuna | 2.62 | 3.07 | 2.72 |
| 18:00 | 5487 | Inter Ibiza CD vs CD Binisalem | 3.61 | 3.08 | 2.00 |
| 18:30 | 1443 | CD Manacor vs PE Sant Jordi | 1.89 | 3.22 | 3.85 |
| 18:30 | 1778 | CD Murense vs Platges De Calvia | 4.33 | 3.56 | 1.70 |
| 18:30 | 4124 | Sassuolo vs Genoa | 1.60 | 4.21 | 5.01 |
| 18:30 | 4237 | Atalanta vs Torino | 1.52 | 4.39 | 5.79 |
| 19:00 | 3076 | CD Torreperogil vs CD Alhaurino | 2.32 | 2.94 | 3.04 |
| 19:00 | 3941 | CD Huracan De Balazote vs AD San Clemente | 2.11 | 3.13 | 3.27 |
| 19:00 | 4206 | Taubate SP U20 vs AA Aparecidense GO | 1.35 | 5.02 | 6.18 |
| 19:00 | 5298 | Uniao FC Iacanga SP U20 vs CE Uniao Abc MS U20 | 3.38 | 3.86 | 1.83 |
| 19:15 | 2315 | Velo Clube Rioclarense SP U20 vs Atletico PR U20 | 6.00 | 4.64 | 1.39 |
| 19:30 | 4629 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs Maccabi Kishronot Hadera W | 1.88 | 3.94 | 3.17 |
| 19:50 | 4997 | Al Shabab Kuwait vs Al Kuwait SC | 6.33 | 4.80 | 1.36 |
| 20:00 | 1905 | Sporting Gijon vs Villarreal | 3.45 | 3.21 | 2.11 |
| 20:00 | 1911 | MS Kiryat Gat W vs Hapoel Marmorek Rehovot W | 1.17 | 6.58 | 10.64 |
| 20:00 | 2814 | RC Deportivo Fabril vs Athletic Arnoia | 1.25 | 5.02 | 9.65 |
| 20:00 | 2840 | Hapoel Beer Sheva W vs Hapoel Nir Ramat Hasharon W | 2.65 | 3.81 | 2.17 |
| 20:00 | 4723 | Zaragoza vs Sevilla FC | 4.03 | 3.14 | 1.97 |
| 20:00 | 5297 | Los Barrios vs Xerez CD | 5.02 | 3.14 | 1.72 |
| 20:00 | 5414 | CD Pozoblanco vs CA Antoniano | 2.15 | 2.99 | 3.33 |
| 20:30 | 1514 | AC Milan vs Roma | 2.02 | 3.64 | 3.44 |
| 21:00 | 4441 | UD Collerense vs Santanyi | 3.04 | 2.94 | 2.32 |
| 21:15 | 1733 | Gremio Novorizontino SP U20 vs Santa Cruz PE U20 | 1.92 | 3.61 | 3.32 |
| 21:15 | 4579 | Nova Iguacu FC RJ U20 vs Criciuma - SC U20 | 1.81 | 3.86 | 3.48 |
| 21:30 | 2022 | Bnot Netanya W vs AS Tel Aviv University W | 9.46 | 6.57 | 1.19 |
| 22:00 | 2065 | Almeria vs Elche | 2.36 | 3.15 | 3.00 |
| 22:00 | 4330 | Atl Mancha Real vs Athletic Bilbao | 11.86 | 5.73 | 1.23 |
| 22:45 | 2533 | Arsenal vs Liverpool | 1.70 | 3.77 | 4.53 |
| 22:45 | 2845 | Fiorentina vs Udinese | 1.58 | 4.21 | 5.22 |
| 22:45 | 3809 | Juventus vs Napoli | 2.00 | 3.39 | 3.78 |
| 23:00 | 3112 | Gremio Desportivo Sao vs Carlense SP U20-Falcon SE U20 | 3.03 | 3.41 | 2.10 |
| 23:30 | 5376 | Rayo Majadahonda vs Atletico Madrid | 12.84 | 5.53 | 1.22 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# AJIBU: NATAKA NAMBA YA KUDUMU AZAM FC

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji mpya wa Azam FC, Ibrahim Ajibu, ameahidi atapambana ili kupata namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo ambacho amekiri kina idadi kubwa ya wachezaji wenye viwango vizuri.

Akizungumza na gazeti hili huku timu yake ikishiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Ajibu, ambaye amejiunga na Azam hivi karibuni akitokea Simba, alisema changamoto aliyokuwa nayo sasa ni kuzoea mfumo wa timu yake hiyo mpya.

Nyota huyo alikuwa kwenye kikosi kilichoikabili Meli 4 FC ya Zanzibar na kupata ushindi wa bao 1-0

"Kuna vijana wengi kwenye timu nimewakuta na wana uwezo mkubwa wa kucheza mpira, kwa hiyo na mimi ni lazima nipambane ili niingie katika kikosi moja kwa moja, hii inanipa changamoto kidogo, lakini siyo sana, kwa sababu sasa hivi nimekomaa, kipindi kile nilikuwa bado mdogo," alisema Ajibu.

Kiungo huyo ambaye ni zao la kikosi cha pili cha Simba (Simba B), aliwahi kupelekwa kwa mkopo Mwadui FC ya Shinyanga lakini alirejeshwa mwaka 2017 huku ilipofika 2019, akatimkia kwa wapinzani wao, Yanga.

Alikaa kwenye klabu hiyo kwa msimu mmoja, akarejea nyumbani Simba, mpaka Desemba 30, mwaka jana alipojiunga rasmi na Azam FC.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya vijana wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano mbalimbali kwenye Uwanja wa JMK Park jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga Princess yasaka heshima*

**Na Saada Akida**

KUELEKEA mechi ya watani wa jadi, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema anahitaji kupata heshima na kuondoka na pointi tatu muhimu katika mechi dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.


Edna aliliambia gazeti hili amefanyia kazi mapungufu yao yaliyojitikeza katika mchezo uliopita dhidi ya JKT Queens ili yasijirudie katika mechi ijayo ambayo wanakutana na watani zao.

Kocha huyo alisema ana imani mchezo huo wa 'dabi' utakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja anahitaji kupata pointi tatu muhimu katika kila mechi na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi.

"Tunaendelea na maandalizi ya michezo iliyopo mbele yetu ukiwamo dhidi ya Simba Queens, ni mechi kubwa na ngumu kwa sababu wapinzani wetu nimewaona wako vizuri, tunajiandaa kwenda kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo," alisema Edna.

Aliongeza amewaangalia vyema wapinzani wao na muda uliobakia kabla ya kukutana ni kujipanga kutumia ubora na madhaifu ya Simba Queens ili kujiweka kwenye nafasi ya kuondoka na matokeo mazuri.

Katika mechi ya mwisho timu hizo zilipokutana msimu uliopita, Simba Queens ilipata ushindi wa mabao 3-0 huku ule wa mzunguko wa kwanza wakitoka suluhu.



Michezo
Alhamisi Januari 6, 2022
Nipashe



Tuchel aendelea kumchunia Lukaku UKURASA 21

# SIMBA SC YATIKISA ZANZIBAR

## ●●● Sakho, Bwalya waongoza 'mauaji' katika...



Kiungo wa Simba, Hassan Dilunga (jezi nyekundu), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Selem View FC katika mechi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Aman, Zanzibar jana. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: SIMBA SC**

**Na Adam Fungamwango**

IKIWACHEZESHA wachezaji wawili kwa majaribio, Msudan Sharaf Eldin Shiboub na Cheick Moukoro, raia wa Ivory Coast, Simba ilianza vizuri mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa kuifunga Selem View mabao 2-0 katika mechi ya hatua ya makundi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar jana.

**Yalikuwa ni mabao ya wachezaji wa kigeni, Pape Sakho kutoka Senegal na Mzambia Rally Bwalya.**

Ilichukua dakika sita timu kufika langoni kwa mwenzake na walikuwa ni Selem View, walipopiga hodi golini kwa Simba baada ya Masoud Said kupiga shuti pembeni mwa uwanja, ukagombewa na wachezaji wa pande zote mbili na kama ungeguswa, ungeweza kuleta hatari, lakini mpira huo ukatoka sentimeta chache.

Nahodha wa Simba, John Bocco, alipata pasi safi kutoka kwa Mzamiru Yassin, lakini alishindwa kuukwamisha mpira wavuni akiwa na kipa wa Selem View dakika ya 14 ya mchezo, huku kona iliyopigwa na Rally Bwalya dakika ya 20 ikileta kizaazaa langoni mwa wapinzani wao na Saido Kanoute alikuwa mtu wa mwisho kuupiga, lakini mpira ukapaa juu.

Sakho akiwa kwenye kiwango cha hali ya juu kama ilivyokuwa kwenye mechi dhidi ya Azam FC Jumamosi iliyopita, ndiye aliyeipatia Simba bao la kwanza dakika ya 24 baada ya krosi iliyopigwa na Gadiel Michael kutoka winga ya kushoto ambao kwanza ,Bocco aliukosa na kumkuta mchezaji huyo aliyeusukumizia wavuni.

Baada ya Simba kupata bao hilo, Selem View walionekana kuhama golini na kuanza kufanya mashambulizi langoni kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara, huku presha hiyo ikisababisha kukaribia kujifunga wenyewe dakika mbili tu baada ya bao kuingia.

Mpira mrefu ulipigwa golini mwa Simba, ulimkuta, Paschal Wawa ambaye alipiga kichwa kumrudishia kipa wake, Beno Kakolanya ambaye alikuwa ametoka kidogo golini, lakini kwa bahati nzuri alikuwa makini na kuuweka mpira huo mikononi.

Dakika za majeruhi kabla ya kipindi cha kwanza, mpira ulipigwa kichwa na Bocco, lakini uliokolewa kabla haujavuka mstari wa goli.

Kipindi cha pili, ndicho Simba ilichowaingiza wachezaji wake, Shiboub ambaye ameshawahi kuichezea timu hiyo na Moukoro ambaye alikuwa kivutio kwa dakika 15 alizocheza kutokana na kuwa mwepesi, mwenye kasi, kupiga chenga na mashuti, akitumia mguu wa kushoto.

Bwalya aliipatia Simba bao la pili dakika ya 52 kwa shuti la mbali akiwa pembeni upande wa mashariki na mpira ukaenda moja kwa moja wavuni na kumwacha kipa Yusuph Abdul Ally, akiruka kuokoa shambulizi hilo bila mafanikio.

Abou Rashid, Haroub Bakari waliingia kwa upande wa Selem View, huku Stephano John na Kassim Ally wakitoka wakati kwa upande wa Simba Kanoute, Jimmyson Mwanuke, Dilunga, Sakho walienda nje na nafasi zao kuchukuliwa na Israel Mwenda, Shiboub, Chris Mugalu, Moukoro na Yusuph Mhilu, mabadiliko ambayo yalizifanya timu zote kuchezea mpira kwa pasi fupi fupi na za ufundi, bila kubadilisha ubao wa magoli.

Simba itashuka tena dimbani kesho usiku kucheza dhidi ya Mlandege wakati mabingwa watetezi, Yanga wao wataikabili KMKM kuanzia saa 10: 15 jioni, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Amaan.

## Wanachama Yanga kujiandikisha kisasa

**Na Saada Akida**

WANACHAMA wa Yanga wametakiwa kujisajili upya kupitia Kampuni za Kilinet na N-Card ili kupata idadi kamili ya wanachama hao kwa ajili ya kusaidia kutambua thamani ya nembo ya klabu yao ambayo inaelekea katika mfumo wa mabadiliko ya kiuendeshaji, imefahamika.

Yanga iliingia rasmi mkataba na Kilinet pamoja na N-Card katika kufanikisha mchakato huo wa usajili wa kisasa.

Kuelekea mfumo wa mabadiliko, klabu ya Yanga imebakiwa na hisa asilimia 51 na kiasi kingine kilichobakia cha asilimia 49 kitakwenda kwa mwekezaji atakayepitishwa.

Akizungumza jijini jana, Mkurugenzi wa Fedha wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema viongozi wa matawi watatakiwa kufika klabuni na kununua vitabu vya fomu pamoja na nakala ya katiba ya klabu ili kutambulika rasmi.

"Mwanachama ataenda kwenye tawi lake, atajaza fomu kwa ada ya Sh. 2,000 akiwa na picha mbili, baada ya hapo atajaza fomu na kulipa Sh. 29,000 ambapo Sh. 24,000 ni ada ya mwaka mzima na Sh. 5,000 itakuwa kwa ajili ya kodi," alisema Mfikiriwa.

Alisema baada ya hapo vitabu kutoka matawini vitarudishwa klabuni na kitakachofuata ni Kilinet kuzipeleka taarifa za wahusika kwenye mtandao na kila mwanachama atapata ujumbe wa kwanza kabla ya N-Card kuthibitisha amesajiliwa rasmi na kujulishwa namba yake ya uanachama.

Naye Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, Hersi Said, alisema hatua hiyo ya mwendelezo wa mchakato wao wa mabadiliko ambao walianza nayo na sasa wanaelekea hatua za mwisho.

"Kila mwanachama na shabiki anatakiwa kujiunga, na wale wote ambao wako katika makundi ya WhatsApp, hawatakuwa na ruhusa kuchangia jambo lolote la Yanga hadi watakapoonyesha au kuthibitisha wao ni wanachama waliothibitishwa," alisema Hersi.

Wakati huo huo, Msemaji wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema mchezaji wao mpya, Crispin Ngushi, tayari ameshajiunga na kikosi cha timu hiyo kilichoko kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi huko Zanzibar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P